

**Neuro
Linguistic
Programming
(NLP)**
An Indispensable Tool in
Coaching

**KU-UPROGRAM UBONGO ZAIDI KWA AJILI YA
UTENDAJI ZAIDI KIMAISHA**

MUANDAAJI NI: MAADHI A.R - +255764244867

www.bakwataonlineacademy.ac.tz

Table of Contents

SEHEMU YA KWANZA	5
UBONGO WA MWANADAMU NA UWEZO WAKE MKUBWA.....	5
Namna ya kutumia ubongo vizuri	6
MIFANO YA KUJIZOEZA VITENDO VYENYE FAIDA KUBWA NA KISHA VIKAWA TABIA YAKO	6
SEHEMU YA PILI	7
SEHEMU YA TATU	10
SEHEMU YA NNE.....	13
JUHUDI NA MAARIFA ULIPA SANA.....	13
KUMBUKA SHETANI HAPENDI LOLOTE ZURI KWAKO.....	15
SEHEMU YA TANO.....	16
Program maalum za UBONGO ukilala	16
Program za UBONGO ndotoni.....	16
Ndoto imegawanyika sehemu kuu 3.....	17
Ndoto za ujumbe maalum.....	17
REJEA QUR'AN uone ndoto yenye ujumbe maalum.....	18
Ndoto zisizo nzuri kimaisha.....	18
Kuna ndoto nyingi za aina tofauti.	19
SEHEMU YA SITA:.....	21
DHIKIR sahihi inavyoongeza nguvu ya ubongo kubuni na kuboresha maisha	21
Kila mtu anaandika kitabu chake cha maisha bila kujua.	21
Kitabu cha maisha yako kiko mikononi mwako.....	22
SEHEMU YA SABA.	23
KUUPROGRAM UBONGO KUWA NA TIJA KIUTENDAJI ILI KUBORESHA MAISHA KIMWILI, KIROHO NA KIUCHUMI	23
Law of Attraction (Kanuni ya Mvutano)	25
SEHEMU YA NANE.....	27
SEHEMU YA TISA.....	30
Law of Attraction na Telepathy katika KUUPROGRAM UBONGO WAKO	30
Telepathy ni nini?.....	30
Ulishawahi kuona yafuatayo?	30
Nguvu ya mvutano(Law of Attraction).....	31

SEHEMU YA KUMI	34
SEHEMU YA KUMI NA MOJA	35
UWEZO MKUBWA WA UBONGO KATIKA KUTUNZA TAARIFA	35
Kifo na usingizi ni kama ndugu!	35
TELEPATHY NA YANAYOJIRI USINGIZINI	35
MUNGU MMOJA WA PEKEE upokea roho wakati wa usingizi pia!,	36
Mtu akifishwa roho inachukuliwa na pia akisinzia roho inachukuliwa!.....	36
Nini Falsafa ya usingizi, ndoto na UBONGO katika maisha ya kila siku?.....	36
SEHEMU YA KUMI NA MBILI	37
SEHEMU YA KUMI NA TATU.....	40
SHETANI HUVURUGA UBONGO KWA KUKALIA CONTROL CENTRE	41
SEHEMU YA KUMI NA NNE	42
Njia za kulinda UBONGO	45
Matamshi.....	45
SEHEMU YA 15	46
SEHEMU YA 16.....	48
ALLAH.....	48
Namna ya kutumia jina Allah KUUPROGRAM ubongo	50
SEHEMU YA KUMI NA SABA	51
Kutumia majina mazuri ya Allah KUUPROGRAM UBONGO	51
SEHEMU YA KUMI NA NANE	54
SEHEMU YA KUMI NA TISA	56
SEHEMU YA ISHIRINI	58
SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA	60
SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI	62
DUA MAHSUSI YA DHATI.....	62
SEHEMU YA ISHIRINI NA TATU	64
Dua ni silaha ya Muumuni.....	65
SEHEMU YA ISHIRINI NA NNE	67
SEHEMU YA ISHIRINI NA TANO	69
SEHEMU YA ISHIRINI NA SITA	73
SEHEMU YA ISHIRINI NA SABA	75


USHUHUDA WA KISAYANSI WA KWELI WA MADHARA YA UBONGO ULIOVURUGWA NA MARADHI YA AJABU	76
USHUHUDA WA KWELI, USOME KWA MAKINI	76
SEHEMU YA ISHIRINI NA NANE	81
UBONGO WAKO ULINDE USIVURUGIKE AU KUVURUGWA	81
SEHEMU YA ISHIRINI NA TISA	88
UBONGO UKIVURUGWA NA MARADHI, MAWAZO YASIYO NA MAJIBU(STRESS) NA MFAZAIKO(DEPRESSION) USABABISHA MWILI MZIMA KUATHIRIKA.	88
SEHEMU YA THELATHINI	92
Vyakula vinavyoongeza nguvu za ubongo na uwezo wa kukumbuka	92
Vyakula hivi si vizuri kiafya na ubongo wako utakuwa dhaifu ukizoea kuvila	97

SEHEMU YA KWANZA

KUUPROGRAM UBONGO ILI UWE NA TIJA ZAIDI KIUTENDAJI

UBONGO WA MWANADAMU NA UWEZO WAKE MKUBWA

Neuro Linguistic Programming (NLP)



Tendo lolote likirudiwa mara nyingi basi ubongo ulichukua na kuwa Tabia ya mhusika.

UBONGO una sehemu mbili za kutunza vitendo na habari muhimu. Sehemu hizo ni:

1. **Conscious mind**
2. **Subconscious mind**

Tabia na taarifa ya kudumu iko ndani ya Subconscious mind.

Tabia na taarifa za muda ambazo upotea kwa muda mfupi utunzwa kwenye conscious mind.

Ukiwa umelala UBONGO uendelea kufanya kazi kama kawaida na Subconscious mind uwa bize kuchakata taarifa mbali mbali zilizoingia siku kabla ya kulala.

ALLAH ALIYETAKASIKA ni muweza wa yote, hajampa mwanadamu elimu nyingi ila kampa kidogo tu!

Kamfundisha mwanadamu machache sana katika mengi. Mwenyezi Mungu anaelekeza kumuomba muda wote kila lolote zuri ikiwemo Elimu yenye manufaa

Rabbi zidni ilma ni sehemu aya ndani ya QUR'AN ikionyesha elimu inaongezwa kwa kila mhitaji kama anaitafuta na kujifunza kwa dhiti.

Mambo yasiyoonekana kwa macho ya mwanadamu ni mengi sana kuliko tunayoyaona hapa duniani.

Laiti tukiona yasiyoonekana katika mazingira yetu tungeona maajabu na mengi ya kutisha!

Lengo kubwa la mifano Hiyo ni kukwambia kwamba UBONGO wako na wa kwangu ni hazina kubwa sana endapo itatumiwa vizuri.

Namna ya kutumia ubongo vizuri

1. Kutenda mazuri yenye manufaa kwako na jamii kwa kutaka rehema za ALLAH.
2. Kuiga tabia za waliofanikiwa kama Mtume Muhammad REHEMA NA Amani ziwe juu yake ili nawe ziingie ubongoni upate faida hapa duniani na kesho Akhera.

Namba 1 na 2 hizo juu ndio Neuro Linguistic Programming yaani NLP kuprogram ubongo wako upya kwa kuuzoeza tabia muhimu na nzuri kimaisha na jamii pia. Kulazimisha UBONGO kukamata mambo muhimu ya maana ni jambo kubwa kimaisha na hii ndio NLP.

Nchi zote zilizopata maendeleo na zenye watu wenye vipaji zinafundisha kozi hii ya NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING.

Yaani namna ya kuprogram ubongo kuwa na tija zaidi kiutendaji kwa kuulazimisha kupokea na kufanyia kazi matendo ya kimafanikio na kuufanya usipokee upuuzi na kuutupilia mbali ukiingia ndani ya ubongo.

MIFANO YA KUJIZOEZA VITENDO VYENYE FAIDA KUBWA NA KISHA VIKAWA TABIA YAKO

1. Ukijilazimisha kuamka saa 11 kila siku kwa Alarm , baada ya siku kuanzia 11 hadi siku 21 mfululizo na ukaacha Alarm utashangaa kila ikifika saa 11 asubuhi unaamka bila kuamshwa na Alarm wala mtu yoyote. SUBUHANNA LLAH. Hii sasa itakuwa tabia na itatunzwa kwenye ubongo wako.

Ukizoea kulala saa 3 jioni na ukafanya hivyo kila siku baada ya siku kuanzia 11 hadi 21 utashangaa ikifika saa 3 unapata usingizi hata ukiwa kwenye kiti umekaa.

Ukijizoeza kutochelewesha kazi yoyote bila sababu utashangaa unakuwa mwenye kutenda mengi kwa muda mfupi.

Ukizoea kuandaa shamba mapema na kupanda mazao kwa wakati, basi itakuwa tabia yako kujiletea maendeleo. ALHAMDULILLAH tulazimishe UBONGO kusoma QUR'AN, kufanya dhikir, ISTIGHFAAR, kutoa sadaka hata tende 1 au korosho 1 au karanga, na hata kikubwa tukiwa nacho .

Tulazimishe UBONGO kusali swala kwa wakati za faradhi na sunna, kuwa mbele katika kujitolea kwenye heri.

Tulazimishe UBONGO kuwajibika


Tulazimishe ubongo kuwa bize na ya kwetu kuliko ya wengine

Tulazimishe UBONGO kuacha fitina husuda ya kuumiza wenzetu kwa husuda uunguza moyo wa mwenye husuda. ALLAH tusamehe na tuepushe fitina na shari za husuda.

Lazimisha UBONGO kufikiri sana na kugundua fursa za kimaisha kwa manufaa yetu na jamii . Allah hana kinyongo kwani ni ARRAHMAN, Allatuif, Alkariim, Almujib, Arrahiim, Arrazak.

UBONGO UPO KWA AJILI YAKO NA NI ASETI YAKO ILAZIMISHE KUIFUNZA YALIYO MUHIMU UTAONA FAIDA KUBWA.

UPROGRAM UBONGO KWA TABIA MUHIMU NA UTAPOKEA INSHAAALLAH



SEHEMU YA PILI

UWEZO WA UBONGO NA JINSI YA KUUPROGRAM ILI KULETA MAFANIKIO
MAKUBWA KATIKA MAISHA YAKO
(NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING)

الْمُحْسِنِينَ نَجْزِي وَكَذَلِكَ ۖ وَعِلْمًا حُكْمًا آتَيْنَاهُ وَأَسْتَوَىٰ أَشَدَّهُ بَلَّغَ وَلَمَّا

(AL-QAS'AS' - 14)

Na Musa alipo fika utu-uzima baraabara, tulimpa akili na ilimu. Na hivi ndivyo tunavyo walipa walio wema.

Somo KATIKA aya hiyo???

Unapewa Akili kwanza kisha ndo elimu

Ukiwa na elimu bila akili ni tatizo.

Ni bora kuwa na akili kuliko kuwa na elimu bila akili.

Nabii Musa alipewa Akili kwanza na kisha elimu. Ewe ALLAH tuzidishie akili na ELIMU

(AL-QAS'AS' - 24)

Basi Musa akawanyweshea; kisha akarudi kivulini, na akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayo niteremshia.

Katika Aya hiyo??Musa alitoa msaada bila kuombwa na wala hakudai malipo, alisaidia tena watu wasiojulikana kwake, kwa kupeleka mifugo yao kunywa maji kwani walikuwa wanasubiria wenye nguvu wachungaji wamalize kunywesha ya kwao nao wapeleke mifugo yao pale kisimani.

Kwa hiyo Nabii Musa aliwasaidia na wakarudi nyumbani mapema bila kukaa pale kisimani kwa muda mrefu kama siku zote. Msaada wa Musa ulimpa Musa malipo makubwa baadaye kutoka kwa baba yao aliyewatuma wakamuite huyu Mtu mwema aliyetanguliza msaada bila masharti.

UPROGRAM Ubongo wako kwa kuiga hii tabia ya Musa ya kusaidia kwanza bila kutaka malipo ili watu waone uwezo wako na kama wakijifanya hawaoni MUNGU atawaonyesha wengine waje wakupe ujira.

Watu wengi hawataki kujitolea kwanza ili waonyeshe uwezo wao na kisha wapate zaidi, watu hawataki kutengeneza huduma kwanza ili ijulikane bila kutaka malipo bali wanatanguliza kila kitu kuambiwa watalipwa nini?

Tunaona sasa hivi kuna PROGRAM za KOMPYUTA unapata free na nyingine pesa kidogo unalipia.

Hawa wanaotoa huduma bure baadaye wanakuwa matajiri kwa kupata wadau wengi na Kisha kuanza kuchangia.

Mfano WhatsApp ni bure , Facebook ni bure, Instagram ni bure, google search engine ni bure, yaani unasikia mtu anasema unagoogole na kupata Habari [?][?] Youtube bure, n.k.

Lakini wote hao wenye kuanzisha facebook, Instagram, youtube, Google, Yahoo, .nk ni matajiri sana na wanaingiza mabilioni kila siku kwani wanapata pesa kwa kuhudumia kwanza.

Mfano facebook unajisajiri bure, unatumia bando lako kisha unafurahi kupata marafiki na kusoma post zao pia unaweza kutangaza kiasi biashara yako bure. Sasa ukitaka kutangaza kwa wengi utalipia tangazo kwa wiki au mwezi au mwaka au Siku moja kwa watu wengi wa eneo utakalotaka na hapo ndipo utalipa na wakapata pesa , hata Instagram wanapata kupitia matangazo ya kulipia na youtube hivyo hivyo. Pia whatsapp wanayo business WhatsApp.

Ila wote wanatoa huduma bure kwanza kwa wengi na kisha wanapata sana baadaye bila gharama kubwa na kwa wepesi.
Hiyo ni Kanuni ya nabii Musa MJA WA ALLAH.

NABII MUSA ALIPOWAS Aidia BILA KUTAKA MALIPO KWANZA, YALITokea YAFUATAYO

(AL-QAS'AS' - 25)

Basi mmoja katika wale wanawake wawili akamjia, naye anaona haya. Akasema: Baba yangu anakwita akulipe ujira wa kutunyweshea. Basi alipo mjia na akamsimulia visa vyake, alisema: Usiogope; umekwisha okoka kwenye watu madhaalimu.

Sasa hapa Nabii anaombewa ajira ugenini??. Unaona kusaidia kwanza au kujitolea kwa dhati kunavyolipa?

Soma hii AYA ??

(AL-QAS'AS' - 26)

Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yetu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu.

Ukijifunza tabia hizo hapo juu na ukalazimisha ubongo wako ukazizoea utashangaa ufanisi utakaopata. Hii ndio NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING

KUPROGRAM UBONGO KUPOKEA TABIA NZURI KWA KUJIFUNZA KWA WALIOFANIKIWA WAKIWEMO MITUME , MASWAHABA, VIONGOZI, MATAJIRI NA WATU MASHUHURI WALIO ACHA MANUFAA KWA WENGI.

VITENDO VYA NABII MUSA HAPO JUU AKIWA UGENINI VILIMLIPA SANA. TUIGE NASI KUSAIDIA BILA KUTANGULIZA UJIRA TUTAPATA ZAIDI YA MATARAJIO.

SEHEMU YA TATU

KUPROGRAM UBONGO YAANI NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING



Kuwa na Kichwa kikubwa au ubongo mwingi si kigezo cha kuwa na akili kisayansi.

Pia kuwa na akili si kigezo cha matumizi ya akili hiyo. Unaweza kuwa na akili lakini usiitumie ipasavyo kutokana na hulka yako na mazingira unapoishi. Akili isiyotumika ni kama Dhahabu iliyo ardhini na haijulikani kuwa ipo.

NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING ni kuboresha akili yako kwa kuufundisha ubongo vitendo vya kuamsha akili iliyo lala.

Unaweza ukamtambua mtu mwenye husuda mbaya kwa vigezo vitatu

1. Kuona neema aliyopata mwenzake akabadilika sura hadi akapata homa
2. Kuongea vibaya kuhusu neema hiyo ya mtu hadi akamchukia na kuanza kumsema vibaya
3. Kukaa kimya na akiombwa ushauri hayuko tayari kushauri wala kuwa karibu na nduguye aliyepata neema hata kwa usaidizi wa kuisemea neema hiyo.

Moyoni kuna mengi na vichwani mwetu kuna mengi yanayofikiriwa kila sekunde!

Tunayosema mdomoni ni wastani wa asilimia 7 tu! Asilimia 93 zote ziko sirini kwa maana kifuani na kwenye fikira.



Hii hatari kwani mtu anaweza kuwa anaongea na kucheka mbele yako ila ni zaidi ya nyoka!

Ukijifunza jinsi ya KUUPROGRAM Ubongo utapata dalili za kujua wengine kitabia na kujihadhari nao na wewe utafanikiwa kwani utaacha tabia za husuda, fitina na maradhi mengi ya kudhoofisha nafsi.

Nilishuhudia mhasibu mmoja mwenye CPA anasaini cheki ya malipo ya mfanyakazi ili asafiri nje ya nchi kupata mafunzo ya siku 10 na baada ya hapo huyu mhasibu aliugua ghafla akaomba ruhusa kwenda kulala. Mimi nilipowauliza wanaomjua vizuri kuhusu kuumwa ghafla na kutetemeka wakasema ndo zake, amepata husuda na akiipata uwa anaugua siku 1 hadi 3 kisha anakuwa sawa!

Unajua kwa nini?



Kwa sababu UBONGO wake kauprogram vibaya!

Hawa wanaomjua pia wanatumia akili zao kwa dalili na matukio ya kuugua watu wakifanikiwa au kusaini cheki za wenzake! Yote hiyo ni Neuro Linguistic Programming

Soma QUR'AN

Upate kujua mengi ikiwemo KUUPROGRAM ubongo wako kuwa bora na kutumia akili uliyozawadiwa na Arrahman.



(AL - A'NKABUT - 35)

Na tumeacha katika mji huo Ishara ilio wazi kwa watu wanao tumia akili zao.

Kuna Ishara nyingi za matukio ya kila siku mijini na vijijini ila wengi hatujifunzi kwa kutazama Ishara hizo.

Katika Aya hiyo juu tunaona ALLAH anasema wanaotumia akili zao

Kwa ufupi kuna funzo kuwa kuna wenye akili ila hawazitumii akili hizo. Ikiwa hubadiliki, huachi mazoea basi akili zako hauzitumii!

KUUPROGRAM ubongo kwa kufanya dhikir, kusoma QUR'AN, ISTIGHFAAR, kutafakari maumbile ya dunia, jua , sayari, mimea inavyoota kutoka ardhini baada

ya mbegu moja kuoza kwanza kisha ikatoa mmea na mazao mengi hiyo ndio kukuza uwezo wa Ubongo na akili kutumika.

Ukipanda mbegu 1 ya mahindi kisha ikaota na kuwa mmea kisha ikatoa mashuke 2 na ukavuna na ukakuta mbegu nyingi zaidi ya 200 unajisikiaje? Au unafikiri vipi kwa muujiza huu?

Ukitumia akili utaongeza ucha Mungu, utasema ALHAMDULILLAH, utatoa zaka na sadaka.

Kuufunza UBONGO tabia za KIMAENDELEO, kiucha MUNGU, kufikiri kwa kina na kukuza vipaji vya utambuzi kwa kuuboresha ubongo ndiyo lengo kuu la NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING (NLP)

SEHEMU YA NNE

KUUPROGRAM UBONGO ILI KUONGEZA TIJA KATIKA MAISHA

JUHUDI NA MAARIFA ULIPA SANA



Soma Aya hii

(AL - A'NKABUT - 69)

Na wanao fanya juhudi kwa ajili yetu, Sisi tutawaongoa kwenye njia zetu. Na hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na watu wema.

ALLAH ALIYETAKASIKA muweza wa yote anasema kila juhudi ya heri yeye uiongoza. ALHAMDULILLAH.

Juhudi yenye kuambatana na maarifa bila kukosa subira ulipa duniani na Akhera.

Vipi juhudi yenye maarifa itapatikana?

Katika mfululuzo wa somo la Kuuprogram UBONGO (Neuro Linguistic Programming) ili kuongeza tija katika maisha tumeona kuwa ukijizoeza matendo fulani kwa kipindi cha muda wa kuanzia siku 11 hadi 21 inakuwa tabia. Inategemea vitendo gani unajizoeza kisha vinakuwa tabia. Kama ni kusoma QUR'AN na DHIKIR baada ya kumaliza swala basi itakuwa tabia yako na utahisi msukumo kila siku wa kusoma QUR'AN bila kuikosa, pia dhikir.

Ukijifunza tabia za watu wema na ukajizoeza nazo basi baada ya muda utashangaa inakuwa tabia yako.

Maana ubongo unauprogram kwa kurudia rudia vitendo hivyo muhimu kimaisha utakuwa hivyo hivyo.

Unaweza kusoma kitabu chenye kuelekeza stadi za maisha na UKIJARIBU kwa vitendo mara nyingi na mwisho wa siku utakuwa na stadi hizo kimaisha na kufaidika wewe na jamii.

Kundi la marafiki uigana tabia, hii inategemea tabia zipi wanazo wengi wao.

Kundi likiwa na tabia mbaya litazalisha watu wenye tabia mbaya wengi! Ndio maana wanasema ukitaka kujua tabia za watu Fuatilia marafiki zao wanaokaa nao, kutembea nao kwa muda mwingi.

UBONGO unauprograma kwa kuona, kutenda, kuongea na kuiga,



Kuna michezo ya kuigiza yenye kuonyesha vita, mauaji, kufyatuliana risasi. Imeprogram vijana wengi hadi Ulaya wanafunzi wamewaua wenzao kwa kuchukua bunduki za wazazi wao na kuwamiminia risasi kiurahisi kwa mambo madogo tu! Hii ni kwa sababu ya programming ya ubongo kwa kuona michezo ya kikatili na kuzalisha tabia za kikatili kwa baadhi ya watazamaji!

Mauaji yanazidi kuongezeka hata nchini mwetu, baadhi ya watu hawana huruma na ubongo umecopi tabia za kikatili.

KUUPROGRAM UBONGO wako kwa kuiga vitendo vya watu waliofanikiwa, watu wema kama manabii, maswahaba, wacha MUNGU ni jambo muhimu sana kwa kila mwanadamu.

Pia ukijifunza tabia za wafanyabiashara waliofanikiwa kwa kuwajibika na kuiga kanuni zao za kibiashara utafikia kiwango cha kutenda mengi kama wao kwani UBONGO utakuwa unaprogram kwa kanuni mpya.

Ukiwa KIONGOZI na ukajifunza tabia za uongozi na utawala bora za VIONGOZI waliofanikiwa na ukazizoea kivitendo basi na wewe utakuwa KIONGOZI aliyefanikiwa.

Maisha yana kitabu kikubwa sana kisichoonekana na karatasi zake ni nyingi ila haziishi ukiwa bado uko hai!

Unaweza andika mengi mazuri kwa muda mfupi kwenye karatasi tupu za kitabu chako cha maisha!

KUUPROGRAM Ubongo kila mara kwa tabia nzuri na bora ni kujiongezea thamani hapa duniani na Allah aliyetakasika kwa rehema zake atakulipa na msamaha wake ni matumaini ya kila mja mwenye kuamini.

Ukijizoeza Kuswali Tahajud mfululizo kuanzia ziku 11 hadi 21 basi itakuwa tabia labda ukikatisha tena bila kuswali kwa siku 11 hadi 21 hiyo tabia ya heri inafutika unakuwa mzito kuamka.

Ukijizoeza kusoma QUR'AN na Kumtaja ALLAH kila siku baada ya muda inakuwa tabia na ukiacha kwa muda huo huo inafutika Hiyo tabia ya heri.

KUMBUKA SHETANI HAPENDI LOLOTE ZURI KWAKO



Shetani AMEAHIDI kumuwinda mwanadamu kila kona ili asiwe BORA ZAIDI katika heri.!!

Au'dhubillah Minasheitwani Rajiim .

Omba Dua na Kusoma Qur'an kila siku ili Shetani asikutawale kifikira

SEHEMU YA TANO

Program maalum za UBONGO ukilala



(AR-RUM - 23)

Na katika Ishara zake ni kulala kwenu usiku na mchana kutafuta kwenu fadhila zake. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao sikia.

Program za UBONGO ndotoni

Katika sayansi ya neurones na Ndoto (Neuro science of dreams) kuna muujiza mkubwa katika sayansi ya ndoto!

ALLAH AKBAR, SUBUHANNA LLAH , ALHAMDULILLAH

Mwanadamu akilala analala yeye tu, ila moyo haulali na UBONGO haulali.

Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mmoja wa pekee aliyetakasika ambaye akitaka lolote liwepo usema kuwa na hapo hapo linakuwa anatoa mengi muhimu kupitia baadhi ya ndoto tangia kale. Kujua tafsiri ya ujumbe wa ndoto ndio kazi kubwa kwa mwanadamu

Sehemu za UBONGO kama Subconscious uwa kazini kupanga na kuchakata habari muhimu za mhusika aliyesinzia.

Kuna ujumbe upitia ndotoni kwa baadhi ya wanadamu ila kuna wanaosahau ujumbe huo yaani ndoto! Kuna wanaokumbuka kidogo na wengine wanakumbuka ndoto nzima.

Maisha ya wanadamu kwa asilimia 33 yote anakuwa usingizini.

Kawaida katika masaa 24 yaani siku 1 inabidi ulale masaa 8 kiafya au 7 ikiwa chini masaa 6.

Kwa hiyo kwa miaka 60 utakuwa umelala miaka 20.

Kwa hiyo usingizi ni maisha, ndoto nyingi ni ujumbe muhimu kimaisha ingawa ukiota unaona kawaida. Laiti tungefuatilia ndoto ungepata afya bora, unge boresha maisha na ungegundua mengi .

Ndoto imegawanyika sehemu kuu 3.

☒Ndoto za mawazo yako

☒Ndoto za woga

☒Ndoto za ujumbe maalum uliombatana na jumbe za kiroho(Spiritual messages)

Ndoto za ujumbe maalum

Hizi ni muhimu kuzifuatilia katika maisha kwani zina ujumbe maalum na ukijua tafsiri yake kwa kiasi Fulani utakuwa makini au utabadilisha mfumo wa maisha.

REJEA QUR'AN uone ndoto yenye ujumbe maalum

[YUSUF - 36]

Wakaingia gerezani pamoja naye vijana wawili. Mmoja wao akasema: Hakika mimi nimeota nakamua mvinyo. Na mwingine akasema: Mimi nimeota nimebeba mikate juu ya kichwa changu, na ndege wanaila. Hebu tuambie tafsiri yake, kwani sisi tunakuona wewe ni katika watu wema.

Hao walipoota walifuatilia kwa nabii Yusuf alipokuwa gerezani nao Aliwapa tafsiri.

Mmoja alimwambia utasamehewa , kweli alisamehewa na akawa karibu na mfalme na huyu mwenzake wa ndege kula kilichopo kichwani alimwambia kuwa utahukumiwa na kusulubiwa , kweli alihukumiwa kusulubiwa na ndege walidonoa kichwa chake baadaye.

Ndoto zinaprogram ubongo na ndo maana wanasayansi wengi waligundua kupitia ndoto, watu wa tiba uota dawa na zikitumika uponyesha wagonjwa.

Kuna ndoto za ajabu ila ukiziota unaona kawaida na haufikiri kwa kina, Ukifikiria ndoto na kufuatilia maana utaepuka mengi na utaboresha mengi na hii nayo ni KUUPROGRAM UBONGO kwa kufuatilia ndoto za ujumbe maalum.

Ndoto zisizo nzuri kimaisha

1. Kuota unapaa
2. Kuota unakula au unapewa vyakula au vitu usivyojua ukale?
3. Kuota unafanya tendo la ndoa mara kadhaa
4. Kuota uko chooni, bafuni, sehemu chafu?
5. Kuota unajisaidia
6. Kuota nyoka mara kwa mara, wanyama , paka, nbwa na pengine wanakufukuza
7. Kuota unagombana na watu
8. Kuota mvua ya mawe na radi au ya mawe tu au radi tu
10. Kuota mafuriko
11. Kuota waliokufa mnaongea mara kwa mara
12. Kuota una watoto usio wajua , kama ni mwananke ananyonyesha, nk
13. Kuota unavuka mto na wakati mwingine unatumbukia
14. Kuota uko baharini au ziwani mara kadhaa au uko ufukoni.

Kuna ndoto nyingi za aina tofauti.

Kumbuka mitume na waja wema walipokuwa wanaota ndoto za ujumbe MAALUM walikuwa wanazifuatilia na kuzifanyia kazi bila kuchelewa na hapo wanapata kitu kimaisha au tahadhari. Yote hii ni **KUUPROGRAM UBONGO** kupitia ndoto ili MAISHA yawe bora ZAIDI.

Mfalme wa Misri aliota ndoto ya ng'ombe 7 wanene na ng'ombe saba wamekonda, mashuke saba mabichi na mengine makavu. Aliangaika mpaka akapata jibu kutafsiriwa na Nabii Yusuf kisha Yusuf akatoka gerezani na kupewa cheo kikubwa cha kusimamia hazina zote za uchumi wa Misri kwa kutafsiri ndoto hiyo ya Mfalme. Hiyo ndo nguvu ya KUUPROGRAM ubongo kuwa bora zaidi na kukupa daraja duniani na kesho Akhera. Yusuf alisimamia kilimo na miradi ya misri ili kujiandaa na janga la njaa kwa miaka 7. Misri ilipata uchumi mkubwa na watu wakawa wanakuja kununua chakula Misri. Lakini CHANZO cha mafanikio ni kuifanyia kazi ndoto ya mfalme. NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING kupitia Ndoto moja ilipaisha uchumi wa Misri na Nabii Yusuf na ukoo wake wakawa na HESHIMA nchini Misri.

Soma aya hizi upate funzo zaidi la UMUHIMU wa kuota na kufuatilia ndoto zako kwa makini

[YUSUF - 43]

Na siku moja mfalme alisema: Hakika mimi nimeota ng'ombe saba wanene wanaliwa na ng'ombe saba walio konda. Na mashuke saba mabichi na mengine makavu. Enyi waheshimiwa! Nambieni maana ya ndoto zangu, ikiwa nyinyi mnaweza kuagua ndoto.

[YUSUF - 46]

Yusuf! Ewe mkweli! Tueleze nini maana ya ng'ombe saba wanene kuliwa na ng'ombe saba walio konda. Na mashuke saba mabichi na mengine makavu, ili nirejee kwa watu wapate kujua.



[YUSUF - 47]

Akasema: Mtalima miaka saba kwa juhudi. Mtacho vuna kiwacheni katika mashuke yake, isipo kuwa kidogo mtacho kula.

Baada ya nabii kutafsiri ndoto hizi alipewa cheo cha heshima na akaandaa mpango mkakati wa uchumi wa kilimo na ufugaji kisha kuusimamia na maghala yalijaa chakula kukabiliana na miaka 7 ya balaa kubwa ya ukame na njaa kwani mazao yasingestawi. Misri ilikuwa na uchumi imara hata wakati wa njaa. CHANZO ni kuifanyia kazi ndoto ya mfalme. Mfalme kama angeamka na kunyamaza ingekuwa tabu kwa taifa zima la Misri.

SEHEMU YA SITA:

DHIKIR sahihi inavyoongeza nguvu ya ubongo kubuni na kuboresha maisha



Sayansi ya UBONGO inaonyesha kutamka maneno ya aina fulani kwa kuyarudia mara nyingi kwa muda mrefu usaidia KU UPROGRAM ubongo kuwa na nguvu mpya inayosaidia mhusika kuwa bora zaidi kiutendaji na kifikiria kwa tabia za maneno anayotamka mara kwa mara


Kwa mfano ukitamka sana majina mazuri ya ALLAH kama Arrahman, Arrahiim, Al MALIK, Al AZIIZU, Al Hakiimu utashangaa unacopy sifa za majina hayo kichwani na tabia yako inakuwa na sifa ya maana ya majina hayo.

1. Subhan Allah
2. Alhamdulillah
3. La ilaha ill'Allah
4. Allahu Akbar
5. Astaghfirullah
6. La Hawla Wala Quwwata ila Billah
7. Subhan Allahi Wa Bi Hamdihi
8. Subhan Allahil Adhim

Kila siku tamka maneno haya, Dhikir, tena kila neno mara 11 au zaidi hata x 100. Allah atakupa heri na msamaha kisha utaboresha ubongo wako zaidi.

Muhimu katika kutamka uwe makini na kuzingatia maana halisi ya DHIKIR unayotamka. Hakika kumtaja Allah ni jambo kubwa.

Maisha ni zaidi ya umri. Umri ni miaka tu, lakini maisha ni kitabu chenye mengi ya kuisimua, kufurahisha, kusikitisha na kufundisha nafsi yako na wengine.



Kila mtu anaandika kitabu chake cha maisha bila kujua.

Kuna vitabu viwili vya maisha kwa kila mtu.

Kitabu cha kwanza ni

☒Kitabu kinachorekodiwa kila mema na mabaya ya kila mtu, kitabu hiki kiko kwa ALLAH . Kitabu hiki hakuna anayekisoma duniani isipokuwa siku ya Kiyama kitasomwa mbele ya kila mhusika.

☒Kitabu kinachoandikwa na wewe kila siku kwa matendo yote unayofanya ila hakiko kwenye karatasi wala KOMPYUTA bali kiko kichwani mwako na nafsi yako inakisoma na jamii baadhi ya kurasa inazisoma kila kukicha.

Kitabu cha maisha yako kiko mikononi mwako

Mfano ukisaidia kulisha mayatima, maskini, wajane, n.k yote haya yanaoneka na ni mazuri. Mfano ukizini, ukaloga, ukafitini, ukaiba, n.k yote haya ni makosa unayajua na unafanya kwa siri ili wanadamu wasikuone ila Mungu anakuona. Yote hayo ni kitabu chako .

KUUPROGRAM UBONGO kuwa bora ni juu yako mwenyewe kwa manufaa yako.

Unaweza kufanya mengi kwa muda mfupi kwa kufanya mambo zaidi ya mawili kwa wakati mmoja na hii inaitwa "MULTI TASKING"

Mfano unaweza ukawa unaendeaha gari na hapo hapo unamtaja ALLAH kwa sifa zake, lakini muda huo huo unakuza uwezo wa Ubungo kuleta tija kimaisha .

Mfano mwingine unaweza kuwa unaandaa kitabu na hapo hapo unarekodi sauti ya matamshi ya kitabu hicho na hapo hapo video ya mtoa sauti na muda huo huo watu wengi wanasikiliza na kuona kupitia mtandao.

KU UPROGRAM UBONGO WAKO KUWA BORA ZAIDI NA KULETA TIJA KIMAISHA YAANI NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING ni jambo muhimu sana na kila MTU anaprogram kila siku bila kujua anapokuwa kwenye kazi zake au hata akiwa amelala yuko ndotoni.

KILA SIKU NI FURSA YA KUBADILISHA MAISHA YAKO , USIKINAI NA REHEMA ZA ALLAH ALIYETAKASIKA

SEHEMU YA SABA.

KUUPROGRAM UBONGO KUWA NA TIJA KIUTENDAJI ILI KUBORESHA MAISHA KIMWILI, KIROHO NA KIUCHUMI

Mwanadamu alipokea Amana kubwa kwa kukubali na kuahidi kuibeba kwa kutekeleza maagizo ya Allah ila Milima, Ardhi, Mbingu na vyote vilikataa comitiment hiyo, MWANADAMU kasema leta kwangu. Kisha kashindwa. Ushahidi huu hapa??



Soma Aya hii kwa makini

(AL-AH'ZAB - 72)

Kwa hakika Sisi tulikadimisha amana kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Lakini mwanaadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhaalimu mjinga.

Mwanadamu kapokea ila kapuuzia mkataba wa kuipokea Amana. Allah tunakuomba utusamehe na utuwezeshe tutekeleze.

MWANADAMU amepewa cheo kikubwa cha Ukhalifa na kukubali amana kubwa yaani Qur'an ya Allah aliyetakasika.

UBONGO wako una nguvu sana kuliko tunavyofikiria , mwanadamu mwenye akili sana hajawahi kutumia uwezo wa UBONGO wake wote! Aliyetumia kiwango cha juu hajawahi kufikia hata asilimia 20 ya Ubungo. Yaani Genius hatumii ubongo wake zaidi asilimia 20.

Wenye akili sana wanatumia 9 asilimia tu.

Sasa hizi asilimia zaidi ya 80 zikitumika inakuwa faida kwa mhusika na jamii.

Kuna wanadamu walioboresha UBONGO wao na ALLAH akawapa maarifa ya kutengeneza mitambo ya ajabu na nyenzo za kusaidia jamii.

Mfano:

- 1.Ndege za kusafiria
- 2.Simu janja na satélite
- 3.Compyuta
- 4.Mitambo ya kilimo ya kisasa
- 5.Vifaa vya kupima mwili afya kama MRI, T SCAN, MICROSCOPE, N.K
- 6.ROBOT
- 7.ARTIFICIAL INTELLIGENCE TOOLS
- 8.MIFUMO YA KIELECTRONIC KAMA POS , CAS, N.K
9. REMOTE SENSING APPS
10. INTEGRATED CHIPS ZA HALI YA JUU ZENYE DATA ZILIZO NA UWEZO WA KUENDESHA MAMBO MENGI ZENYEWE BILA MWANADAMU KUZIONGOZA

Arrahman kafundisha mengi kwa wanadamu walio tayari kutumia UBONGO wao ipasavyo.

KUUPROGRAM UBONGO ni kuuzoeza tabia sahihi zilizoratibiwa na kisha usiache kuulazimisha kila siku kujiandaa kutenda.

Mfano ukitamka majina ya ALLAH kama:

Al A'lim, Alatuif, Al fattahu mara nyingi na kudhamiria kupewa maarifa yenye manufaa kwa kuwajibika kutekeleza kanuni za kutenda yale unayotaka basi utashangaa unapata uwezo wa kuyatenda na njia za kuyapata zinapatikana na unayapata .

Kuna watu wanaangaika na jambo sana bila kukata tamaa mwisho wanalipata. Hii ina maana ukiangaika unakuwa nalo kichwani masaa 24 mpaka UBONGO unazoea na unakuwa na bidii bila kuchoka mpaka unatenda na linatokea ulitakalo.


ALHAMDULILLAH kuna siri katika KUUPROGRAM UBONGO wako.

Dhana ndani yako yaweza kuzaa kitu,sasa inategemea dhana gani unafikiria muda wote, ukifikiria kushindwa muda wote, usitegemee kufanikiwa. Ukifikiri ushindi

basi utashinda kwani ALLAH ALIYETAKASIKA yuko ndani ya dhana yako. Hii iko ndani ya Hadith sahihi inasema : ALLAH yuko ndani ya dhana ya mja. Dhana yako yatosha kuwa dua yako. Dhania kufanikiwa kifamilia, kikazi, kiuongozi, kimaisha utafanikiwa ili mradi juhudi na maarifa visikose.

Law of Attraction (Kanuni ya Mvutano)

Kila unachowazia sana muda wote bila kuacha basi unakivuta kwako . Basi wazia heri na mafanikio utapata.



Kila kitu kinachooneka mwanadamu amefanya kinaanzia kwenye fikira ndani ya ubongo , mfano

Jengo la GHOROFA 11 , lilianza wazo, kisha mchoro, kisha ujenzi na mwisho jengo refu la ghorofa 11 linaonekana

Fikira uvuta kama sumaku

Chuo kikuu chochote, inaanza wazo, kisha ardhi, kisha mchoro, kisha plan na andiko , kisha ujenzi na kisha walimu na kozi za kufundisha, ndipo chuo kikuu tunakiona.

Chuo kikuu chochote, inaanza

Ndege ya abiria au ya kivita, ilianza wazo tena mtu mmoja kisha mchoro, kisha uundaji na test kisha ndege inapaa.

Sasa hayo yote ni kuumiza kuchwa sana ili yatokee.

Kufikiri ni kugumu ndio maana wanafunzi WENGI wanafeli hesabu kuanzia shule za msingi hadi chuo KIKUU, SI Afrika tu bali hata Ulaya, America, Asia, n.k

Hesabu ni namba na fikiri zaidi kwa kina bila kukata tama, tambua kuwa hesabu inaitwa Lugha ya sayansi.

Lakini kila mtu akiuprogram UBONGO wake kwa kuuzoeza kufikiri basi unakuwa na uwezo mkubwa sana.

Ondoa husuda ubongoni, fitina, kufuatilia maisha ya watu kwa shari, ushirikina, ulevi, ulaji riba na vinyongo.

Upe nafasi Ubongo kwa kuacha yasiyofaa kutunzwa na kuyapa nafasi yaliyo msaada katika UBONGO utafanikiwa mengi.

Mwenyezi Mungu aliyetakasika anasema Hawezi kubadilisha yaliyoko kwetu mpaka TUBADILISHE yaliyo nafsini mwetu.

Ina maana tuna mengi yanatutesa au tunakwama , kuyaondoa ni kujikagua na kisha tatizo letu tunalitafutia chanzo na kukiondoa kwanza ndipo Mwenyezi Mungu atatupa uwezo wa kuyaondoa na kuyaacha kwa kuomba msamaha na kutubu kisha kubadilika.

Kwa mfano mtu ni mzinifu na anapata matatizo ya kila siku ya kufumaniwa, magonjwa ya zinaa , watoto nje ya ndoa na wanaleta kwake mpaka kushindwa hata maisha yake na familia kisha analalamika bila kuacha kuzini na kutubu, unadhani hii itamsaidia tatizo kutoka?

Mfano unakula vyakula vya mafuta zaidi, wanga zaidi na kila nyama iliyonona wewe ndio chaguo lako. Mazoezi hufanyi na huachi kula holela, ukipata ugonjwa wa presha na kisukari kisha unalalamika kuwa huoni na wakati hapo hapo huachi ulaji wa bila mpangilio na kujali afya yako, hii itakusaidia kupona magonjwa bila kuacha kula hovyoy?

Kwa hiyo badili tabia zako mbovu ndipo Mwenyezi Mungu aliyetakasika ataondoa madhara yanayokusibu

Khalifa ni cheo Kikubwa na kushukuru ni kutenda mema na kuboresha fikira zetu kwa kutenda mazuri na kuiga mengine mazuri kila siku na hii ndio KUUPROGRAM UBONGO WAKO ILI KUONGEZA TIJA KATIKA MAISHA KITAALAMU NI NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING.

SEHEMU YA NANE

KUUPROGRAM UBONGO WAKO ILI KUONGEZA TIJA KATIKA MAISHA

Mwanadamu anatumia muda mwingi kujifunza kuhusu vitu kuliko wajibu wa kuumbwa kwake na kujijua yeye mwenyewe!

Soma QUR'AN ﴿﴾



[ADH-DHAARIYAAT - 56]

Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.

[YA-SIN - 78]

Na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atakaye ihuisha mifupa nayo imekwisha mung'unyika?

Tafakari hii aya ya QUR'AN ﴿﴾

[LUQMAN - 28]

Hakukuwa kuumbwa kwenu, wala kufufuliwa kwenu ila ni kama nafsi moja tu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.

Mwanadamu anajifunza sana shuleni na vyuo kuhusu vitu bila kujifunza kuhusu Yeye mwenyewe!

UBONGO wako KUUPROGRAM ukatambua sababu za Kuumbwa mwanadamu,



Sababu za Mwanadamu kuzaliwa na kuishi kisha kufariki na akishafariki kipi kinaendelea!

Kila kitu ulichonacho kinatengenezwa kiwandani na kuna mitambo inayozalisha nguo ulizovaa sasa hivi, simu yako, saa yako, kikombe chako, kiatu chako, gari lako, kitanda chako, n.k Je wewe kiwanda chako kiko wapi?

Jibu Kutoka ndani ya Qur'an

“Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji. ”
(23:12-14)

Na akasema Aliyetukuka: “Amekuumbeni kutokana na nafsi moja. Kisha akamfanya mwenziwe katika nafsi ile ile. Na akakuleteeni wanyama wa mifugo jozi nane. Anakuumbeni katika matumbo ya mama zenu, umbo baada ya umbo, katika viza vitatu. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Ufalme ni wake. Hapana mungu isipo kuwa Yeye. Basi nyinyi mnageuzwa wapi?” **(39:6)**

Kila kitu kinatengenezwa kiwandani kisha kuuzwa na kutumika!

Je wewe na Mimi tumeumbwa kushi tu basi na kisha kufa?

Hakuna la ziada kweli la kuumbwa Sisi?

Kiwanda cha simu yako hii unayotumia hujawahi kufika na ukaona zinavyotengenezwa ila unaamini kuwa kipo na mainjinia wapo ndo maana simu inapatikana dukani na wewe unanunua. Je mwanadamu si zaidi ya simu?

Vyote vifaa wewe ni mtengenezaji kupitia fikira za ubunifu ndani ya UBONGO wako. KUUPROGRAM UBONGO ni tija zaidi kwani kila jambo la ugunduzi linaanzia ubongoni.

Je mainjinia na wafanyakazi wote wa kiwanda cha kutengeneza mwanadamu unawajua?

Jamani tumbo linatoa watu wema, wazuri na wabaya pia ! Wote chanzo ni maji dhaifu yatokanayo na tendo la raha za watu wawili mke na mume na hapo ndio uzalishaji wa kiumbe anayeitwa mtu.

Mwanadamu ni zaidi ya kompyuta na mashine zote za ajabu.

Kujifunza ulivyo na unauprogram zaidi kwa kujifunza mengi muhimu kwa kusoma QUR'AN na Mafunzo ya mitume na tabia zao ndio kujiprogram kimaisha na utafaa zaidi hapa DUNIANI na Mwenyezi Mungu atalipa juhudi yoyote nzuri InshaaAllah.

Tafakari kiwanda cha magari na kazi ya gari kwa mwanadamu.

Gari ikiwa mbovu mara kwa mara inauzwa au inakuwa scrapers.

Je mwanadamu asipomtii aliyemtengeneza na kumkadiria auzwe? Au awe scraper?

Jisome zaidi ya unavyosoma vitu vingine utaboresha ubongo wako zaidi ya sasa.

Kila siku ni nafasi kwako kujisoma zaidi kama khalifa hapa duniani.

Mfano injinia anajifunza uinjinia kuanzia sayansi na hesabu kisha kanuni za uinjinia miaka zaidi ya 17 kama ataishia digrii ya kwanza.

Hapo nimehesabu kuanzia primary hadi chuo Kikuu.

UBONGO wake anaujaza kanuni na wengi wao ukiwauliza kuhusu lengo la kuumbwa kwao utashangaa hawajui!

UBONGO ukiujaza kanuni za Uhasibu, uinjinia, udaktari, ukulima, uvuvi, uendeshaji ndege na kanuni chungu nzima bila kujijua wewe kwanza basi ubongo wako haujauprogram kwa tija.

Jifunze kanuni za vitu na jifunze wewe ni nani na kwa nini uko hapa duniani ili utende kwa weledi kila jambo la kimaisha kwa mujibu wa kuumbwa kama khalifa.

Anasema Mwenyezi Mungu aliyetakasika

[ADH-DHAARIYAAT - 56]

Nami sikuwaumba majini na watu isipokuwa waniabudu Mimi. (Lengo kuu ni kuniabudu)

SEHEMU YA TISA



Law of Attraction na Telepathy katika KUUPROGRAM UBONGO WAKO

Telepathy ni nini?

Ni mawasiliano ya mawimbi yanayotokana na fikira katika Ubongo zilizoratibiwa na uwezo mkubwa wa ARRAHMAN muuba wa kila kitu.

Law of Attraction ni nini?

Ni kanuni ya mvutano utokanao na kuwazia sana kila kitu au jambo kila mara, unapowazia sana kwa muda mwingi basi mazingira ya kutokea au kupata au kufanikisha unachoangaikia yanatokea kimaajabu kwa uwezo wa Muumba wa kila kitu.

Ulishawahi kuona yafuatayo?

Ukimfikiria mtu sana, unashangaa anapiga simu au anatokea

Ukimwambia nilikuwa nakufikiria sasa hivi naye anaweza kukwambia alikuwa anakufikiria au anakuongelea!

Ukiwa unatafuta kitu sana au bidhaa utashangaa habari za kitu hicho au bidhaa zinakuja mara kwa mara na utaona hata matangazo kila sehemu ukienda au utasikia watu wanaongelea kitu hicho au bidhaa hiyo!

Hiyo na mifano mingine mingi ni nguvu ya kitu inaitwa mawasiliano ya ubongo na ubongo kama unavyoona unampigia mtu simu mtu inaita na anapokea.

Telepathy ukiwazia sana mtu kwa umakini naye anapata call ndani ya ubongo anaanza kukuwazia atakapokuwa popote duniani. SUBUHANNA LLAH

Asili ya wanadamu iko hivyo, kuna watu wakiongelewa bila kuwepo wanahisi hali si kawaida kimwili na kifikiria na utasikia mtu anasema kuwa: " Kuna watu wananisema mahala"

Unaweza kufika mahala ukahisi nywele zinasisimka au woga bila sababu, lakini unashangaa ukiwauliza wenyeji wanasema kuwa makini na sehemu hiyo au unaona cha kukutisha pale mfano nyoka, mbwa, mwizi, n.k.

Yote hayo ni nguvu ya maumbile yenye ujumbe wa ajabu na hadi wanasayansi wanaangaika kuyafanyia kazi ili wafaidike na nguvu hizi!

Basi tumia fikira chanya kuvuta yaliyo mazuri na hii ndiyo mojawapo ya KUUPROGRAM UBONGO WAKO ILI KUONGEZA TIJA KATIKA MAISHA yaani Neuro Linguistic PROGRAMMING

Nguvu ya mvutano(Law of Attraction)

Katika fikira ni ubongo na moyo vikishirikiana kuwezesha kiumbe kuzalisha anachofikiri sana muda wote! Kinachokushughulisha sana utokea kwani Mwenyezi Mungu anasema Yuko ndani ya Dhana yako! ALLAH AKBAR, ALHAMDULILLAH, SUBUHANNA LLAH

Muumba wa kila kitu yuko ndani ya fikira zako! Fikiria vibaya kila jambo utapata matokeo mabaya SIKU zote.

Ndiyo Qadar yako ikiwa kuwazia kushindwa basi muda wote utashindwa.

Mwenyezi Mungu ALIYETAKASIKA anasema kuwa hapotezi juhudi ya mwenye juhudi

Hii ina maana kuwa juhudi yako ikiwa ni kukata tamaa, kuona kila jambo haliwezekani, kuona kila saa unaonewa, kulalamika tu bila kuchukua hatua, na mengi yasiyo na tija basi utapata matokeo hafifu au utafeli kila kitu kwani ndo juhudi yako hiyo.

Lakini ukiwa unafikiri na kujaribu bila kukata tamaa na ukiendelea kutawakali kwa ALLAH ALIYETAKASIKA utashangaa juhudi yako inazaa matunda na ndio ufanisi unapatikana.

Nguvu ya mvutano yaani Law of Attraction ina makubwa katika kuboresha uwezo wako kwa kila nyanja za maisha.

Watu wenye tabia tofauti wakikaa kambi kwa muda wa mwezi 1, utashangaa wanaanza kuwa na makundi hata kama kabla ya kuja kambini hawakujuana!

Ukifuatilia makundi yaliyojitokeza utakuta yana tabia watu wenye tabia zinazofanana kwa kiasi kikubwa!

Utakuta watu wenye kupenda mpira wako karibu kujadili mechi

Utakuta wataalam wa Afya nao wameishajuana na kupeana Ushauri na uzoefu

Utakuta wa dini fulani wameishakuwa karibu na utashangaa ni kundi

Utakuta wafanya biashara nao wameisha kuwa na kundi lao

Utakuta wavuta sigara wameishajuana na wako karibu na wanashirikiana

Utakuta watu wenye tabia ya fitina nao wako karibu na wameishaanza kuvuruga kambi na wanashirikiana vizuri kuvuruga

Utakuta wezi wameishajuana pia, wazinifu pia, wachawi pia.

Yote hiyo ni Law of attraction.

Baada ya kambi utashangaa makundi kibao kwa tabia zao!

Wakitawanyika kuna watakaokuwa wameongeza ujuzi au uzoefu kutokana na kundi la watu wenye tabia sawa alilokuwemo.

Uzoefu unatofautiana na hii inaweza zalisha wengi wenye tabia nzuri au mbaya.

Mfano: ukikaa muda mwingi na wavuta sigara kuna uwezekano wa kuvuta zaidi yao au kama huvuti tambua Moshi unaathari kwako sana!

Kama unakaa muda mwingi na wauza marashi , tambua kuwa utafaidika harufu nzuri na utanunua na hata usiponunu a watakupulizia kidogo au utakuwa una enjoy harufu ya marashi ukiwa nao.

Mifano hiyo na sigara na marashi ni mfano halisi wa marafiki na watu tunaokaa nao au watoto wetu wanaokaa nao au wake, waume wanaokaa nao muda mwingi.

Kutokana na KUUPROGRAM UBONGO tunapashwa tupate kuwatafuta watu walio na tabia nzuri, waliofanikiwa na kukaa nao japo kwa masaa 2 kwa wiki na hata ukibahatiwa masaa 2 kwa siku au kuishi nao Karibu ili tuathiriwe na tabia zao nzuri za kimaisha.

Kama hawapo tulipo basi tusome historia zao na kutenda mara nyingi nasi tutakuwa tumebadilisha fikira zetu na kuwa bora zaidi kimaisha.

Mfano ukitaka kuwa msomaji wa vitabu vya maarifa mengi, basi anza kusoma hata ukurasa mmoja kila siku, na utacopy tabia ya kujisomea baada ya siku 11 hadi 21 mfululuzo.

Ukitaka kuwa mfanya biashara mzuri, basi Angalia wafanya biashara waliofanikiwa na WASOME kwa makini na wewe fanya mara kadhaa bila kuacha na utafanikiwa.

Kama unahitaji kuwa mtu wa swala za usiku, funga, kusoma QUR'AN na mengi mazuri. Anza kuamka saa 9 usiku na kusali rakaa 3 tu, na soma QUR'AN sura fupi, kila siku ukifanya hivyo utashangaa unapata hamu ya kusali rakaa 11 usiku na kusoma QUR'AN sura ndefu.

Kwa ufupi UBONGO KUUPROGRAM kwa kuiga tabia muhimu za manufaa kwako ni muhimu sana katika maisha haya ya dunia.

Watu wana stress, mifazaiko, maradhi ya ajabu,kutoridhika, mifazaiko, n.k

UBONGO unauprogram kuwa kila jambo kuna mwisho wake na ALLAH aliyetakasika ndiye muweza, basi utaona kila siku ni fursa kwako hata ukiwa katika Mtihani wa kimaisha.

SEHEMU YA KUMI

Tunazidi kusoma zaidi kuhusu fikira zetu zinavyoathiri maisha yetu ya kila siku, Kuuprogram Ubongo ni muhimu sana kwa sasa kwani mengi ya kuuvuruga yanaongezeka.

Tunazidi kusoma zaidi Telepathy na nguvu yake ya kimuujiza na huu ndio Ukubwa pia wa Mwenyezi Mungu muweza wa kila kitu. ALHAMDULILLAH



Telepathy ni hali ya kufikiria mtu ukiwa mbali na yeye akapokea signal kichwani mwake na kukumbuka na kisha kukufikiria.

Mfano ukimuwazia mtu ghafla ina maana na yeye anakuwazia. Lakini ikitokea mtu akakuwazia vibaya kila mara kama kukuchukia , kukufitini hadi kukusema vibaya

na wewe utanza kumstukia na kujihisi kutokuwa na raha na pengine ukaanza kumuota mnagombana, mko pamoja na mko kimya, n.k.

Inakwenda mpaka kwenye dua , hii ukiombewa ukiwa haupo , athari yake inaingia ndani mwa maisha yako kwa njia hii ya telepathy. Dua ya mtu asiyekuwepo ina nuvu ikiwa wasomaji dua wana nia njema na wametulia.

Kwa hiyo hii telepathy inaendelea katika maisha yetu hata bila kujua. Ukijua sasa utawazia watu muhimu na walio na nia nzuri kwako na utajizua kuwazia chuki na mabaya kiasi kwamba ukiwazia mabaya ulaani Shetani na kujitahidi kuwa na fikira chanya kwa watu walio na fikira chanya.


Ukimuwazia mke wako Vizuri na uko mbali itamuathiri kwa mawazo hayo, ukiwazia rafiki muda mwingi aliyeko mbali itamfikia fikira naye akuwazie hata asipokutafuta au kukupigia simu atastukia anakuwazia.

Ukiwazia mafanikio muda wote kazini, biashara na wajibu wowote basi utashangaa njia zinakuwa nyepesi na unaona njia za kufanikiwa zinapatikana.

Wateja wako watakupenda, ndugu watasogea na maadui watajionyesha. Kuna mengi juu ya telepathy.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

UWEZO MKUBWA WA UBONGO KATIKA KUTUNZA TAARIFA



Computer 1.2 bilioni zenye **Hard disk 1TB** ni sawa na uwezo wa kutunza data wa UBONGO wa mtu mmoja.

Allah Akbar! SUBUHANNA LLAH! Tuongeze juhudi katika kumcha Mwenyezi Mungu, ASTAGHFIRULLAH , ALHAMDULILLAH. Pata Makubwa kutokana na usingizi na UBONGO katika maisha ya kila siku.

Kifo na usingizi ni kama ndugu!

Roho uchukuliwa na ALLAH ukilala na urudishwa ukizinduka usingizini ila wakati mwingine roho hairudishwi na kwahiyo hauzinduki ndipo usema amefia usingizini.

Wengi wamefia usingizini

TELEPATHY NA YANAYOJIRI USINGIZINI

Soma Aya hii ya QUR'AN Tukufu

(AZZUMAR - 42)

MWENYEZI MUNGU huzipokea roho zinapo kufa. Na zile zisio kufa wakati wa kulala kwake, huzishika zilizo hukumiwa kufa, na huzirudisha nyengine mpaka ufike wakati uliowekwa. Hakika katika hayo bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri.

MUNGU MMOJA WA PEKEE upokea roho wakati wa usingizi pia!,

ALLAH AKBAR, SUBUHANNA LLAH

Yaani tukisinzia roho zinapokelewa na Mwenyezi Mungu, na mtu akifa pia vile vile, roho yake inapokelewa na Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu anaamua unafia usingizini kwa kutoirudisha roho unapoamka

Mara ngapi? Unasikia mtu kalala mzima ila wakimuasha hawezi tena! Wakiangalia wanakuta ni maiti tayari akiwa kitandani kwake!!

Hii inakuonyesha usingizi ni jambo kubwa na ndoto ni jambo kubwa. Mtume rehema na Amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alipokuwa anakaribia kulala alikuwa anasoma dua na kujiandaa kama anakwenda safari tena ya kivita. Dua za Kulala , Aya za QUR'AN na kuweka nia ya kuamka usiku kusali. Hayo maandalizi ya kulala yalikuwa ya kimkakati wa hali ya juu.

Kwa hiyo usingizi ni kama kifo kabisa, kwa mujibu wa aya Hiyo hapo juu.

Mtu akifishwa roho inachukuliwa na pia akisinzia roho inachukuliwa!

Roho inarudishwa kwa yule muda ulio bado, na pia inabakizwa na kutotoka usingizini kwa yule ambaye muda wa kuishi umemalizika anafia usingizini!

Nini Falsafa ya usingizi, ndoto na UBONGO katika maisha ya kila siku?

UBONGO na program zake ukiwa umelala na nguvu ya dua na QUR'AN kusomwa kabla ya kulala yote hayo yatafafanulia kwa utafiti kutokana na mafunzo ya Mtume REHEMA NA Amani kutoka kwa ALLAH ziwe juu yake na tafiti za sayansi zilizopo.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

KUUPROGRAM UBONGO WAKO ILI KUONGEZA TIJA KATIKA MAISHA

Kila siku ni fursa kwa kila mtu kubadili mstakabali wa maisha yake.

Tumeona jinsi UBONGO unavyoongoza mengi ya KIMAISHA kuanzia maamuzi na kujenga tabia zinazofaa kimaisha kwa manufaa ya mhusika.

Kila kitendo tunachofanya au neno tunalotamka lina athiri maisha yetu. Inategemea tendo gani umetenda au maneno gani umesema

Soma aya hii kutoka ndani ya QUR'AN, Tafakari.

(FUSS'ILAT (AU H'A MIM SAJDAH) - 46)

Anaye tenda mema basi anajitendea mwenyewe nafsi yake, na mwenye kutenda uovu basi ni juu ya nafsi yake vile vile; wala Mola wako Mlezi si mwenye kuwadhulumu waja.

Ukifikiria mazuri muda wote utauprogram UBONGO wako kwa mazuri.

Maisha yako yataonyesha unachokifikiri kwani mwenye roho safi hata uso wake unonyesha nuru na bashasha original wala si ile ya kufanana na waigizaji.

Mtu anakuwa na uso wenye chuki mpaka unaona kama anataka kulia!

Kichwa kikijaa fikira za matumaini, heri, wajibu wa kuumbwa na kila mara kufikiria mema na kuyatenda basi utakuwa umepata faida kubwa kimaisha kwa sababu utakuwa na utendaji wenye tija kimaisha na kesho Akhera. Mwenyezi Mungu ALIYETAKASIKA anaona kila heri na kila shari. Tujiepushe na shari na tuzidishe heri.

Unapofikiri maovu kwenye UBONGO wako yanaweka makazi, na ukiendelea kufikiri hayo hayo maovu basi inakuwa tabia yako.

Ukifikiri maovu kwa muda mwingi utatenda maovu kwa muda wote!

Tumeshuhudia makundi ya kimaafia na kazi yao ni kuua, kuteka watu, kuhujumu jamii n.k.

Genge la Majambazi linaundwa na wanadamu wenzetu!

Genge la wachawi linatokana na wanadamu wenzetu

Genge la Wafitini linatokana na WANADAMU wenzetu

Kuna mtu na makundi ila tabia zinatofautiana.

Kabla ya kulala unaprogram maisha kwa kufanya yafuatayo:

1. Pata udhu
2. Soma Sura hizi



Bismillah Rahman Rahim



Transliteration

(1) Qul huwa Allahu ahad (2) Allahu assamad (3) Lam yalid wa lam yoolad

(4) Wa lam yakul-lahu kufuwan ahad

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ① مَلِكِ النَّاسِ ② إِلَهِهِ ③
النَّاسِ ④ مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ⑤ الَّذِي
يُوسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ ⑥
مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ⑦

Bismillahir-Rahmanir-Raheem

1. Qul a^udhu birabbinnas.
2. Malikin-nas.
3. Ilahin-nas.
4. Min sharril-waswasil-khannas.
5. Alladhi yuwaswisu fi sudurin-nas.
6. Minal-jinnati wan-nas

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ① مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ② وَمِنْ
شَرِّ خَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ③ وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ ④
⑤ وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ⑥

TRANSLITERATION

Qul 'audhu bi rabbil falaq, min
sharri ma khalaq, wa min sharri
ghasiqin idha waqab, wa min
sharrin nafathati fil uqad, wa min
sharri hasidin idha hasad.

Ikhlaswi, Nnasi na Falaq

Kila ukisoma unapulizia viganjani na kujipaka mwili mzima utakapo fikisha viganja vyako. Utasoma mara 3 , Puliza viganjwa vyako na weka karibu na kinywa na soma

kila ukisoma zote 3, unapulizia viganjani na unajipaka na unafanya hivi mara 3 kisha unalala katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu.

Soma Ayatul Qurussiyu x 1 au zaidi.

Kisha Samehe kila mtu, usilale na kinyongo kwani kusamehe kabla ya kulala ni jambo kubwa sana. Kusamehe ni afya na kuboresha maisha yako. Kusamehe ni kuwa huru na kuupa moyo afya, kuipa nguvu akili na ni kumridhisha Mwenyezi Mungu aliyetakasika kwani yeye ni mwingi wa kusamehe, **SUBUHANNA LLAH. Eti mwanadamu anasema siwezi kusamehe! Wewe nani! Kiburi ni sifa ya Ibilisi Aliye laaniwa.**

Kisha ISTIGHFAAR nyingi na fikiria mazuri ukiendelea kutamka, **Allah, Assalam, Alatuif, Arrahman, Arrahiim**, mpaka usingizi ukuchukue.

Faida ya kujiandaa kabla ya kulala ni nyingi sana. Kubwa ni kuandaa ubongo uwe na power hata ukiwa umelala, pia ni mafunzo ya Mtume REHEMA NA Amani kutoka kwa ALLAH ziwe juu yake.

Ukijiandaa hivyo kila siku kabla ya kulala utaona miujiza ndani ya siku 11 na kuendelea.


Hakikisha MIPANGO mizuri unaiwaza unapomaliza dua zako, dhikir na ukiwa kitandani. Hii itaufanya ubongo utunze ulichowaza zaidi kabla ya kusinzia.

Ubongo kuuprogram kabla ya kulala kuna mengi utayaona ndani ya maisha yako.

SEHEMU YA KUMI NA TATU

Ubongo una mfano wa idara na kila idara ina kazi yake.

Mfano sehemu inayoitwa control centre (CC) , hii ni kuratibu mawasiliano ya milango yote ya fahamu na maamuzi ya nafsi yako.



Ukigusa kitu gizani na ukatambua kuwa ni kitu gani, mfano kikombe, jiwe, kisu, pesa unaweza vitambua kwenye giza kwa kugusa tu.

Hiyo ni control centre iliyowasiliana na viganja vya mkono wako na kutoa ujumbe kwenye ubongo wako kuwa ulichoshika ni kitu cha aina fulani.

Maamuzi yote ya mwanadamu katika kutenda yako ndani ya ubongo na sehemu maalum inayohusika ni CONTROL CENTRE (CC)

Kwa hiyo ubongo wa kila mtu ukiutazama uko na idara sawa ila utendaji ni tofauti kati ya mtu na mtu.

Ikitokea short yoyote kwenye waya za ubongo ndipo mtu anageuka na kuwa kichaa au mwenda wazimu au muuaji asiye na huruma kabisa.

DHIKIR, Kusoma QUR'AN, Sadaka, ISTIGHFAAR, Kumswalia mtume na Funga vinasaidia kuimarisha UBONGO wa kila mwenye kutenda kila SIKU

Mwenyezi Mungu muumbaji wa kila kitu ni rahisi kuupa nguvu UBONGO wako kwa kila jambo unalotaka na likatendeka kimiujiza.

Soma hii AYA YA QUR'AN kisha Tafakari

(AL - AH'QAAF - 33)

Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, aliye ziumba mbingu na ardhi, na hakuchoa kwa kuziumba, kuwa ni Muweza wa kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.

SHETANI HUVURUGA UBONGO KWA KUKALIA CONTROL CENTRE

Mkatalie, Audhubillah Minasheitwani Rajiim.

UNAPOJITAHIDI KUUPROGRAM UBONGO WAKO IBILISI ANAJITAHIDI KUUVURUGA

Shetani uvuruga moyo na ubongo kwa kiwango cha hali ya juu sana.

Ndio maana Mitume Rehema na Amani za ALLAH ZIWE juu yao wote walikuwa wanaomba dua kila mara na kumtakasa na kumtaja ALLAH kwa kuomba ulinzi wake.

Rejea Nyiradi za Mtume rehema na Amani za ALLAH ziwe juu yake za kila mara na kila kitu alichokuwa anataka kufanya ni kuanza na dua hata kama ni kupanda farasi au kuvaa nguo au kuingia chooni.

SEHEMU YA KUMI NA NNE

Hii sehemu ni ya kukuonyesha UBONGO unavyoweza kuvurugwa na watu, mashetani wa kijini na kibinadamu.



Hii ni kweli , soma QUR'AN uone ukweli wake

(ANNAS - 5)

Anaye tia wasiwasi katika vifua vya watu,

(ANNAS - 6)

Kutokana na majini na wanaadamu.

Hizo aya zinaonyesha uvurugaji wa nafsi na ubongo kiasi kwamba umfanya mwanadamu kuwa na wasi wasi na ukikosa utulivu basi na ubongo hautatulia.

Shetani analo group madhubuti la kuvuruga MWANADAMU na kizazi cha mwanadamu. Ushahidi ni ahadi aliyotoa kuwa atatuwinda pande zote na kututia wasi wasi ili atuvuruge vichwa vyetu na tusifanikiwe.

Yeye Shetani kwa kutumia majini wa kishetani ukalia CONTROL CENTRE ya mwanadamu ili kudhibiti maamuzi ya mwanadamu kinyume na utu wake. Pia shetani wa kijini usafiri kwenye mwili popote kupitia mishipa ya damu ya mwanadamu. Udhibiti tabia na maamuzi ya mwanadamu kiasi kwamba atakuwa na tabia tofauti na wengine walio sawa.

Shetani ni mzoefu wa miaka mingi katika upotezaji kwani tangia enzi za nabii Adamu rehema za Allah ziwe juu yake alianza kumpoteza mwanadamu kwenda kinyume na maagizo ya Allah aliyetakasika, sasa miaka mingapi akiwa anapoteza wengi!



Kwa hiyo shetani anao uzoefu wa kupoteza, huwezi ukamshinda kwa kuitwa sheikh au ustaz au aliyesoma dini sana na dunia bali utamshinda kwa kusoma mbinu zake alizokuwa anatumia kujaribu kupoteza mitume lakini mitume walikuwa wanatumia mbinu gani kumshinda Shetani?

Soma mbinu za Shetani za kupoteza na soma jinsi mitume walivyokuwa wanamshinda. Shetani kila siku tunamuona kwa

dalili, mfano unapoanza kusali yanakuja mambo mengi hata ya miaka iliyopita, mpaka yale uliyokuwa umeisha sahai yanaweza kutokea kwenye fikira ukianza kusali! Jua hapo umevurugwa na shetani ili usimuabudu Allah Aliyetakasika kwa khushui na tafakuri ya kutosha.

Unaweza ukaanza kusoma Qur'an na ukaanza kusinzia ukifika katikati ya sura au ukienda kusali ijuma huna usingizi ila wakianza hotuba unaona watu wengi wamesinzia ingawa hotuba ya Ijumaa ndio ujumbe mkuu wa Ijumaa. Ijumaa ikiisha wataanza kuongea na usingizi unapotea. Shetani huyo ni mbinu zake za kukufanya usisikilize ujumbe uliopo kwenye hotuba ya ijumaa au mawaidha.

Shetani unaweza ukamuona kwa dalili ya kuahirisha mambo mazuri ya kiamendeleo bila sababu mpaka wenzako unabishana nao , kwa kusema nitaanza na nguvu zote baada ya wiki au mwezi na hadi unaondoka duniani hufanyi au wanakuondoa kwenye madaraka kama ni kiongozi.

Shetani anachochea hasira kwa mambo madogo, mfano mke na mume wanaweza kuanzia jambo dogo tu na ukashangaa ugomvi mkubwa unaanza na siku hiyo

hawaongei wote hadi kesho yake au wiki. Tena hapo ni afadhali hadi kupigana na kuumizana au kutoleana kashifa mbele ya watoto na majirani kuamua.



Shetani ni adui mkubwa na haonekani kwa macho ila dalili zake ndizo kipimo cha kujua kuwa yupo kazini. Msome zaidi alivyo jaribu kumpoteza nabii Nuhu, Suleiman, Musa, Ibrahim, Muhammad na waja wengine. Njia walizotumia ni kumtegemea Allah aliyetakasika na kujinasibisha na maombi kupitia swala na mema yenye kuendelea. Audhubillah

minasheitwani rajiiim.

Unaweza kuona mtu anasali swala tano ila mzinifu kuanzia madada wa kazi, wafanyakazi wenzake, mtaani, .n.k mpaka mke wake anakosa kuleta dada zake, wasaidizi wa kike kwa kuhofia mume wake ingawa anaswali, na ni msomi wa dini.

Hii yote ni kuwa anazo PROGRAM mbili kichwani mwake ikiwemo ya Shetani.

Wanadamu wanajifunza uchawi na kuutumia kuvuruga ubongo wa watu, kuwazuru na kuwafanyia hujuma zisizoonekana kwa macho ila kwa dalili.



Mtume Muhammad Rehema na amani za Allah ziwe juu yake alishafanyiwa uchawi na mtu mmoja kwa jina **Labid** lakini akagundua mapema kupitia ndoto na Allah akampa maelekezo ya kujitibu kwa aya za QUR'AN na dua.

Kichwa chako ndio msingi wako wa mabadiliko kimaisha, hii ndio sababu ukipanda pikipiki unaambiwa kuvaa Helmet na usipovaa ni faini!

Kichwa hiyo ina ubongo na ubongo unaprogram muhimu kimaisha, linda kichwa chako kwa hali yoyote ile.

Mtu akiwa kichaa wanasema kichwa kimevurugikiwa au waya zimekatika. Kichaa hawampimi miguu wala tumbo bali anapimwa kichwa.

Soma QUR'AN kila siku, Funga , Fanya ibada za usiku, toa sadaka, Taja Allah mara nyingi, Omba MSAMAHA, Tumia majina yake kumuomba kwani kasema yeye anayo majina mazuri kama ARRAHMAN, Arrahiim, Al MALIK, Al qudus, ASALAM, Almuumin, Al Fattahu, Arrazak, Aljabbar , Alatuif,

Kila jina kusudia maana yake na Omba kwalo kwani yeye analinda na ni mlinzi mzuri. Kila jambo kwake lina sababu , sisi wakati mwingine tunaweza tusijue sababu kwa kikomo cha uwezo wetu aliotupa.

Kichwa chako muhimu sana. Kukiprogram ni muhimu na kukilinda kisivurugwe pia.

Njia za kulinda UBONGO

Hiyo Suratil Nasi lengo lake ni kukupa tahadhari na kuitumia suratil Nasi na sura zingine za QUR'AN kama Ikhlaswi, Falaq katika kuomba ulinzi kutoka kwa ALLAH ili Wavuruga moyo na ubongo washindwe kwa jina la ALLAH ALIYETAKASIKA.

Soma Sura hizo kila asubuhi na jioni kuzuia uvurugaji wa moyo wako na ubongo ili wasiharibu akili yako hawa kundi la shetani miongoni mwa majini na watu ingawa utaona kuwa uko sawa.

Dua ya kuomba ulinzi iliyokuwa inasomwa na Mtume rehema na Amani ziwe juu yako.

Matamshi

Soma X 3 hii dua

Bismillahil'ladhi la yadhur'u ma'as-mihi shai'un fil-ardhwi wa-laa fis'samaa;
Wa-hu'waas samii'ul alim

Hii ni kuomba Ulinzi wa Mwenyezi Mungu ili shari yoyote isikuguse. Ulinzi utapata kwani yeye wa pekee ana nguvu kubwa na majeshi mengi.


Hakuna chichote cha kuvuruga ubongo wako kama ukiisoma asubuhi na jioni Kwa dhati.

Arrahman anaweza tumtegemee Sana.

Pia Toa sadaka kwa wahitaji ni kinga.

SEHEMU YA 15

Kuiga tabia nzuri za watu wengine na kuzizoea mpaka zikawa tabia yako ni KUPROGRAM UBONGO wako kuwa bora zaidi.



Hii inaitwa NEURO LINGUISTIC PROGRAMMING

Tunaendelea kujua zaidi na kutumia kanuni za kucopy tabia bora ndani ya ubongo wako ili KUONGEZA uwezo wako wa kiutendaji na kifikiria.

Mtume REHEMA na Amani kutoka kwa ALLAH ziwe juu yake alikuwa akifanya yafuatayo:

1. Anaswali swala tano na ziada ya sunna.
2. Alikuwa anafunga swaumu ktk Mwezi wa

Ramadhani na baadhi ya siku maalum miezi mingine

3. Alikuwa anasoma QUR'AN kila siku na anaifundisha pia

4. Alikuwa anafanya ISTIGHFAAR mara 100 kila baada kusali anasema kwa dhati Astaghfirullah waatubu ileiy x 100

5. Alikuwa anatoa sadaka kwa kiasi awezavyo

6. Alikuwa anakaa na udhu

7. Alikuwa anapenda masikini, mayatima na wajane kwa kuwasaidia na kuwahudumia
8. Alikuwa anaomba dua kila alichotaka kufanya kama kulala, kuingia mji mpya, kula, kuoga, kusafiri, n.k
9. Alikuwa hana kinyongo, husuda ya chuki, Uzembe
10. Alikuwa anasamehe haraka
11. Alikuwa anafanya daawa, yaani anaamrisha mema na kukataza maovu

Hizo ni tabia za Mtume na pia QUR'AN ni tabia yake.




Mimi na wewe tunaambiwa na ALLAH aliyetakasika kuwa atabadilisha yaliyoko kwetu ikiwa tutabadilisha yaliyo katika nafsi zetu.

Tukiiga tabia za Mtume na tukajitahidi kusoma QUR'AN na kufuata maagizo yake tutafanikiwa kila kipengele cha maisha hapa duniani na BAADA YA KUFISHWA.

Hii ndiyo KUUPROGRAM UBONGO kuwa bora.


Ukiiga tabia za wafanyabiashara waliofanikiwa na kufanya kama wao ktk biashara kuna uwezekano mkubwa wa kufanikiwa.

Ukitamka sana na kuwa makini sana majina ya ALLAH ya sifa utaongeza uwezo wa ubongo kwa sifa ya jina hilo unalotamka sana kwa dhati na ukifikiri maana ya jina hilo.



Psyche power ni kuupa uwezo UBONGO kiasi kwamba ukilala unaweza kuota na ukakumbuka ndoto zako kwa kiasi kikubwa, ukaota unapigana na kushinda, ukaota majibu ya changamoto za mchana au za maisha na ukazitumia ukafanikiwa.

Mfano wanasayansi walikuwa wanaota mambo ya ugunduzi na wakijaribu kutenda kama walivyoota wanafanikiwa mfano Benzene ring structure ktk Organic Chemistry iliotwa na mwanasayansi akaamka akaichora kama hexagon.



Neno au maneno unayotamka au kufikiri kila mara yanaathiri ubongo wako. Inategemea unatamka nini na kufikiri nini muda wote. Maneno yana nguvu ya ajabu katika maisha yako. Chagua la kuongea mara kwa mara na acha mengine yasiyo faa kimaisha. Usimlaani motto wako au ndugu ukikasirika kidogo, samehe mara kwa mara. Ongea ufanisi na heri utapata matokeo mazuri wewe na jamii


SEHEMU YA 16

KUTUMIA MAJINA YA ALLAH MAZURI KATIKA KUBOresha UBONGO

ALLAH

Kutumia jina la Allah katika kuuprogram ubongo na kutuliza moyo wako

ALLAH anasema ndani ya QUR'AN kuwa anayo majina mazuri tuombe kwa hayo majina .



Kila jina la Allah lina maana kubwa kiroho na siri kubwa ndani yake endapo litatumika kumuomba Allah wa pekee asiye na MSHIRIKA kwa dhati na kwa muda mrefu bila kuacha. Utaona maajabu yasiyoelezeka endapo utazoea kutumia majina mazuri ya Allah kwa mujibu wa maana ya jina husika.

UBONGO wako utauprogram kwa kutaja jina fulani kwa mujibu wa maana ya jina unalotaja kwa nia na makusudi ya kupata fadhila za Allah kutokana na maana ya jina unalotaja.


Mfano jina ASALAAM

Jina lina maana ya Amani na mleta amani ya kila kitu ni ALLAH yeye wa pekee.

Kama hauna Amani moyoni na kimaisha kutokana na changamoto za kimaisha kama magonjwa, umasikini na mengi yasiyofurahisha.

Jina la As Salam ukilitamka mara nyingi basi Amani na ulinzi wa Allah utahisi ndani yako amani na kujiamini kila utakavyokuwa unazidisha utulivu na kutaja mara nyingi kadiri ya muda wako ulivyo. Taja hata zaidi ya mara 160.

Sasa Tuanze na uwezo wa jina la Muumba wa kila kitu liitwalo



HILI LINAIWA JINA KUU.

Jina hili ni kubwa na ukubwa wake siwezi kuutolea maelezo isipokuwa siri kubwa na ukubwa wake utaupata kwa kutenda maelekezo haya:

Nia ya jambo lolote ni muhimu kiutendaji.

Kila Aamal na nia yake.

Ukiwa na nia ya kuomba MwenyeziMungu kwa kutumia jina lake la sifa na ukafanya muda mwingi na mara nyingi utaona miujiza na siri kubwa kiroho kwani yeye anayo majina mazuri ombeni kwayo.

Muhimu uwe unaswali swala 5 , unasoma QUR'AN, unafanya heri nyingine na kuomba MSAMAHA muda wote .

Namna ya kutumia jina Allah KUUPROGRAM ubongo

Muda wowote tia nia na kukusudia unalotaka kama kupona maradhi, uchumi na riziki ya kutosha, akili na utambuzi, ulinzi, imani na lolote la heri kisha tamka kwa dhati ukiwa umeangalia sehemu moja na unaona jina hilo kama lilivyoandikwa kwenye kichwa chako na uku ukiendelea kutamka hivi

Allah, Allah, Allah, Allah, Allah,.....mpaka zifike 1,000 au zaidi kama utakavyotaka.

Ukiwa unatamka Allah tambua kuwa na UBONGO unakuwa na nguvu ya kujiprogram upya kwa mujibu wa uwezo wa Allah ALIYETAKASIKA.

Allah ni jina kuu la Mwenyezi Mungu ALIYETAKASIKA litumie kwa nia kuombea heri yoyote utaona uwezo wa Allah kupitia jina hilo la kwake lililo kuu kwa hali zote.



Mwingi wa Rehema.

Jina hilo ukilitamka mara nyingi zaidi ya mara 100 kila baada ya swala au muda wowote utakuwa na UBONGO wenye kumbu kumbu na utakuwa na umakini katika mambo yako ya kimaisha na utakuwa mtu mwepesi kwa wengine na hutakuwa na kibri na utawafaa watu wengi.

Rehema za Allah ALIYETAKASIKA zitakuwa nyingi kwako.

Jina la Ar Rahiim maana yake Mwenye kurehemu. Hewa ya Oksijeni ni muhimu sana na kila mtu anaipata free, kula chakula na kikachujwa ili yasiyo faa mwilini yatoke kama uchafu na yanayofaa yatumike kujenga mwili wako yote haya ni Rehema zake ARRAHMAN mwingi wa rehema.

Ukitamka kwa nia na dhati mara nyingi zaidi ya 100 kila baada ya Swala ya Alfajir atapata UPENDO kutoka kwa watu wengi na yeye atakuwa na upendo na kiburi kitatoweka na kuwa na huruma kwa viumbe. Pia majanga ataepushwa. UBONGO wake utakuwa una uwezo na tabia kadiri atakavyokuwa anatamka jina mara

nyingi kila siku kwa maana mambo mengi kimaisha yatakuwa bora na yeye kuwa bora zaidi kwa uwezo wa Allah ndani ya majina yake mazuri ya sifa zake.

Kutenda ndiyo muhimu zaidi kuliko kusoma tu na kisha usitende
Tutaendelea na matumizi ya majina ya Allah ya sifa aliyotuagiza tumuombe kwa kuyatumia.

Mwanadamu mwenye akili nyingi yaani Genius hawezi kutumia hata nusu ya uwezo wa UBONGO wake.

Sasa UBONGO ukitumika vizuri waweze kuona miujiza ndani ya misha yako.

Neuro Linguistic Programming ni kuufunza ubongo tabia fulani mpaka ukawa na uwezo zaidi kiutendaji.

Tabia utunzwa ndani ya UBONGO na kila kumbukumbu pia utunzwa ndani ya UBONGO kwenye sehemu iitwayo Subconscious mind.

Tunza majina ya ALLAH ndani ya UBONGO wako utapendwa na Allah na utakuwa na tabia zenye tija kwa uwezo wa Allah.

Hasbunna LLAH waniima li wakiyl x 11 au zaidi. Dua ni nyenzo muhimu kwa Muislam



ALLAHUMMA swali ala Muhammad. Inapendeza kurudia x 100 au zaidi

SEHEMU YA KUMI NA SABA

Kutumia majina mazuri ya Allah KUUPROGRAM UBONGO

[AL - A'RAAF - 180]

“Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo. Na waacheni wale wanao haribu utakatifu wa majina yake. Hao watakuja lipwa waliyo kuwa wakiyatenda”

Majina yanayojulikana ni 99 ila kuna zaidi ya hayo na anayajua Allah pekee yake hayo mengine.

Sasa tuangalie matokeo na faida ya kuomba kwa kutumia majina haya:

**AL- MALIK,
AL- QUDDUS
AL-MUUMIN
AL-MUHAYMIN**

A-MALIK

Maana ya jina ni Mfalme , yeye ni zaidi ya wafalme wote wa kidunia waliotangulia, waliopo na watakaokuja baadaye.

Jina hili ukilitumia katika maombi kila siku baada ya swala au usiku au muda wowote kwa umakini na nia ya kumtegemea yeye wa pekee Allah ALIYETAKASIKA utaona wepesi katika riziki na heshima kuanzia kwa familia yako, majirani, ndugu, marafiki na watu unaowajua na usio wajua. Utakuwa na sifa za UONGOZI na kutenda kama KIONGOZI.

Jina la Al malik ukikusudia kulitumia katika maombi ya kila siku na ukawa unalitamka mara nyingi kadiri ya muda ulio nao yaani Al MALIK, Al MALIK , Al MALIK, Al MALIK.....zaidi ya mara 100 utaona mambo mengi yanabadilika katika maisha yako.

Kabla ya kuomba dua yoyote, jitathimini kwanza, kisha mswalie Mtume Rehema na amani za Allah ziwe juu yake hivi

**Allahumma swali a'la Muhammad wa alaa alihi Muhammad x 11
au zaidi au zaidi**

Kisha leta ISTIGHFAAR kama hii

Astaghfirullah wa Atubu ilayh x 100

Waombe wazazi wako

Rabi ghfirily waliwaalidaya, rabi rahmuhumaa kama rabayyan swagiirah

Sasa hapa omba dua na ukiwa na yakini kuwa unayemuomba anakuona na yuko karibu yako kuliko hata mshipa wako wa shingo.

Jina la AL-QUDUS

Msafi na mbora zaidi kuliko chochote alichoumba.

Tamka kwa dhati mara nyingi kila siku kwa kutafsiri maana na unachomuomba Allah ALIYETAKASIKA.

Msafi zaidi ya kawaida na utukufu wake hauna mfano.

Jina hili ukilitamka kwa dhati na mara nyingi litakuprogram kuwa mtulivu na mwenye kujizuia na mfazaiko ya kuathiri afya yako. Utakuwa mwenye nafsi isiyo na wasi wasi na utajenga tabia ya kuwa na imani na mipango yako unayo ipanga kwani Allah ndiye Al Qudus atakupa nguvu na uwezo wa kutenda heri kimaisha na utakuwa msingi wa kulipwa heri baada ya kufishwa.

AL-MUUMIN

Mwenye kuzidisha imani , Kila anayemuongoza anakuwa amesalimika.

Ukilitamka mara nyingi jina hilo basi kwa uwezo Allah na kwa nia yako utakuwa na imani zaidi na utalindwa shari, majanga na hatari za wazi na za siri.

Tamka mara nyingi jina hili zuri la AL-MUUMIN , tamka zaidi ya 631 au ifike hiyo.

Kutamka kila kitu sana kuna kazi kubwa ndani ya UBONGO inafanyika kwa sababu neurons zinakuwa na power kwa mujibu wa unachotamka sana.

Sasa ukiomba dua na kuirudia mara kadhaa unachochea malengo ya dua au maombi yatimizwe na Allah.

Malaika wapo wengi na kazi zote wanapangiwa na Allah ALIYETAKASIKA kwani ukiomba MSAMAHA sana kwa kusema Astaghfirullah wa Atubu ilayh unakuwa unafanya jambo kubwa na Kila neno la dua Allah anashuhudia kwa mujibu wa nia yako, pia malaika wanaagizwa watende jambo juu yako. Hakika Allah ALIYETAKASIKA anayo majeshi mengi wakiwemo malaika.

Jina AL-MUHAYMIN

Mlezi au Mlinzi mwenye kujali

Hakuna asiyejua maana na umuhimu wa mlezi mwenye kujali anaye kujali muda wote.

Utampenda naye atakupenda. ALHAMDULILLAH

Jina hili ukijiandaa kwa kuoga, ukasali raka mbili na kumuomba Allah kwa makini na yakini kuwa hashindwi lolote basi utasalimika nje yako na ndani yako. Mlezi wako Allah ALIYETAKASIKA ni muweza wa kila kitu. Subira na kuendelea bila kuacha heri ya kumfurahisha, kumtukuza na kumuabudu ndiyo muhimu katika maisha haya yasiyo halisi na mafupi sana.

SEHEMU YA KUMI NA NANE

KUUPROGRAM UBONGO wako

Majina 99 ya sifa likiwemo jina kuu la Allah yanaprogram UBONGO wa mtu kwa kuyataja mara nyingi na nia mahsusi ya kuyataja kwa kuomba ukitumia jina au majina ya Allah yenye sifa

Soma vizuri aya ifuatayo:

[AL - BAQARA - 220]

--katika mambo ya dunia na mambo ya Akhera. Na wanakuuliza juu ya mayatima. Sema: Kuwatengenezea ndio kheri. Na mkichanganyika nao basi ni ndugu zenu; na Mwenyezi Mungu anamjua mharibifu na mtengenezaji. Na Mwenyezi Mungu angeli penda angeli kutieni katika udhia. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.

Ndani ya aya hiyo hapo kuna majina mawili ya Allah yafuatayo:

AL AZIIZU, AL HAKIIM

Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

Jina **AL AZIIZU** ukilitamka kwa dhati mara nyingi kila mara utakuwa umeuprogram UBONGO wako na wewe utakuwa na uwezo mkubwa kiutendaji na heshima itaongezeka kwa utendaji wako katika kila jambo. Utajisimamia na kuwa mtu anayejali na kusimama imara katika kutimiza wajibu wake.

Allah ameseme ndani ya QUR'AN kuwa anayo majina mazuri, ombeni kwa kuyatumia hayo majina yake.

Utajaliwa uwezo zaidi na utapata matokeo mazuri ya kila dhamira zako nzuri kwani AL AZIIZU AL HAKIM ni muweza na mshindi kwa kila jambo.

UBONGO ulivyotengenezwa na Allah ALIYETAKASIKA unapata nguvu ya ajabu unapotamka MANENO ya kumtukua yeye aliyeutengeneza kwani kila jina lina safirisha nguvu ya mawimbi katika sehemu zote za UBONGO na kila sehemu ya ubongo ina kazi maalum katika utendaji kazi wa mwanadamu.

Ubongo ukibena mawazo machafu ya kihusuda, chuki, ya kwa nini fulani asiwe mimi!? Kuwazia mazuri na mafanikio ndio chakula sahihi cha UBONGO. Kuwa bize na mambo yako ni muhimu sana katika KUUPROGRAM UBONGO.

Mtu yoyote ambaye ana mambo ya kufanya yaliyo muhimu utamkuta ubongo wake una afya nzuri na kadiri anavyofanikiwa ndipo ubongo unakuwa zaidi KIUTENDAJI na kuwa na uwezo mpya na hii ndio KUUPROGRAM hata bila kujua kuwa anauprogram kila anapofikiri mazuri na MAFANIKIO bila kubeba ya watu na kuyaweka kichwani mwake.

Ndio maana viongozi wa dini waliomakini katika ibada na kufanya dhikir mara kwa mara, matajiri, wanasiasa waliofanikiwa huwezi wakuta wanavuruga vichwa vyao kwa mambo yasiyo wahuu wala kuchukia wenzao kwa mafanikio yao wala husuda za kiuadui hawazikaribishi katika maisha yao.

Tajiri, KIONGOZI na yule aliyejikita katika mambo muhimu hawezi kupandisha mapepo kwani Ibilisi hana sehemu ya kukaa, ubongo uko bize na kila idara ina jambo na imejaa.

Kuomba kwa kutaja Majina ya Allah ALIYETAKASIKA, Dhikir za kila kipengele cha utendaji , dhikir za asubuhi na jioni, ISTIGHFAAR, Sadaka , Swala , Funga, Usomaji QUR'AN na Ibada yoyote nzuri ni KUUPROGRAM UBONGO kuwa BORA kiutendaji kwa mhusika endapo atajitahidi kufanya hayo kwa makini na imani kuwa Allah ni muweza wa kila kitu.

SEHEMU YA KUMI NA TISA

KUUPROGRAM UBONGO wako ili kuleta tija kimaisha.

Majina 99 ya Allah yakitumika kwa dhati katika kumtaja na kumuomba lolote zuri na la kheri utalipata. Muhimu ni subira na kutokata Tamaa.

Kukata tamaa na Rehema za Allah ALIYETAKASIKA ni kosa. Usikate tamaa katika kumuomba na kumtegemea Allah mmoja wa pekee asiye na MSHIRIKA.

Jina lolote kwa maana yake halisi ukilitumia kwa dhati kuomba utaona matokeo husika.

Omba kwa majina haya

1. Arrazaq (Mtoa riziki) Alwahhab (Mgawa yote) Allatuif (mpole)
Alfattahu (Mfunguaji), Arrafi'u (Mwenye kunyanyua, kutoa daraja zaidi)

Kwa nia na makusudi ya maana yake ukiomba kwa kuyataja mara nyingi kuanzia mara 100 na kuendelea utapata matokeo tarajiwa katika maisha yako kwa sifa za majina hayo ya Allah ALIYETAKASIKA.

Kumbuka kasema yeye kuwa anayo majina mazuri ombeni kwa hayo majina.

Hayo majina niliyotaja ni majina yenye maana kubwa na sifa zake zimejaa ndani ya majina yote yaliyotajwa ndani ya QUR'AN

Siri ya kurudia mara nyingi katika dua ni kuupa nguvu UBONGO kimaumbile kucopy maana halisi ya unalotaja mara nyingi, pili ni kuwasiliana kiroho kiasi kwamba Malaika wa Allah wenye kupangiwa idara mbali mbali watawajibika kwa hilo unaloomba kwa kutaja mara nyingi kwa amri ya Allah.

Tunaambiwa ndani ya QUR'AN kuwa kuna malaika wengi kwa kazi mbali mbali na hawamuasi ARRAHMAN muumba wa kila kitu.

Mfano kuna malaika wa kutulinda , kuandika matendo yetu ya kila siku, kuna malaika wa kutoa roho zetu, yaani kila jambo limepangiwa malaika, wahusika wawakilishi mpaka kila aya ya QUR'AN, majina na sifa za Allah ktk majina yake.

Ndio maana aya za ulinzi wa Allah zile tatu zinazoanza na Qul..ukisoma maana yake ni kuomba kujilinda kwa uwezo wa Mungu mmoja wa pekee kwa jina kuu ni Allah.

Ayatul Qurusiyu ukiisoma kabla ya kulala mara kadhaa utajikinga na mashetani wa kijini na binadamu. **Kwa nini?**

Kwa sababu maneno yake yamesheheni ulinzi na ponyo.

Kwa hiyo kuna siri kubwa katika majina ya Allah ya sifa zake. Kuna siri kubwa katika kila aya ya QUR'AN.

USISAHAU kukaa na udhu muda wote, kusoma QUR'AN kila siku na maana yake, Kuamrisha mema na kukataza maovu kadiri uwezavyo hata kwa kutuma meseji au kuandika vitabu. kuomba MSAMAHWA yaani Astaghfirullah wa Atubu x 100 au zaidi, kutoa, sadaka, kuwa karibu na ndugu zako, kusali swala 5, kufunga , kufanya Dhikir nyingi , SUBUHANNAH LLAH, walhamdulillah Allah Akbar

Kumbuka Rehema zake Allah zinazidi hasira zake.

Tumieni nguvu ya kiroho iliyomo katika Majina ya Allah ya sifa kumuomba lolote zuri katika dunia hii iliyo na mitihani na mizengwe mingi inayoonekana na isiyonekana

SEHEMU YA ISHIRINI

KUUPROGRAM UBONGO WAKO ILI KUWA BORA ZAIDI

Buy FUTURE Now. at the cheapest price!

Nunua maisha yajayo sasa hivi! Tena kwa bei rahisi!

Soma Aya hii: tafakari siku hiyo!

(AL - FAJR - 24)

Atasema: Laiti ningeli jitangulizia kwa uhai wangu!

Mwanadamu atajuta siku hiyo na kusema angelijua...Majuto ni mjukuu uja baadaye

Tumeona majina ya Allah ya sifa unavyoweza kuyatumia kuupa UBONGO nguvu ya kimiujiza na kuomba lolote kutoka kwa muweza wa kila kitu ALIYETAKASIKA yaani mwenye majina mazuri, anasema tuombe kwa kuyatumia.

ARRAHMAN, ARRAHMAN, AI HAKIIM, AI AZIZU, AI waduud, na majina mengine yaliyotajwa ndani ya QUR'AN yanafaa kuupa UBONGO wako uwezo mkubwa ukiyataja mara nyingi kila siku katika maisha yako.

Ubongo unatoa mawimbi yaani waves yenye kunasa vitu vingi na kupeleka kila sehemu ya mwili.

UBONGO ukitumika vizuri utakuwa bora na Allah utamuabudu vizuri.

Akili ni zao la ubongo kwani ukisikia mtu anasema fikiri ana maana gani?

Kufikiri kunaanzia ndani ya ubongo na kisha matokeo ya fikira uonekana kwa VITENDO.

Kwa hiyo UBONGO wako ukiwa vizuri na ukatuliza nafsi Yako utafanya mambo makubwa katika maisha yako.

Tumia majina ya Allah kuupa ubongo na nafsi nguvu na utulivu mkubwa.

Allahu Ssamadu hii ni sehemu ya aya ndani ya QUR'AN na ukitamka kwa dhati baada ya kila swala, kisha ukamsalia Mtume Rehema na amani za Allah ziwe juu yake na ukaomba MSAMAHA x 100 yaani Astaghfirullah wa Atubu ilayh x100 kisha ukawaombea wazazi wako na waumini yaani " Rabighfirily waliwaalidayya walil muuminina walimuuminat yauma yakuumul hisab, rabbiy rahamhumaa kama rabayyaan swagiirah.

Kisha ukaweka nia yako na kutamka

Allahu Ssamadu x nyingi. Ubongo na nafsi vitakuwa imara kwani maana Halisi kitabia inajitokeza ndani yako kwa mujibu wa uwezo wa Allah.

Imani ni kitu kikubwa! Amini uwezo wa kumuomba Allah kwa dhati na utaona matokeo mazuri. Kuna siri kubwa ndani ya kila jina la Allah la sifa na kila aya ya QUR'AN.

Dunia ni sayari ya,3 katika mfumo wa sayari zinazozunguka jua yaani solar system.

Sisi tuko ndani yake ila kuna sayari kubwa kuliko dunia na hatujui uko kuna nini. Allah anaweza kila jambo na kuna siri nyingi katika maumbile haya ya dunia iliyo ndogo kulinganisha na sayari , nyota zaidi ya dunia.

Tutumie muda huu wa uhai kwani ni zaidi ya mtaji tunaajua sisi.

Kuna mengi hatuyaoni kwa macho ndani ya dunia hii. Wanadamu wengi duniani wamesinzia ila wataamka wakifa.

Yaani tukifa ndo tunaona zaidi na mengi tuliyokuwa tunaona kama ndoto kwa kusoma ndani ya Qur'an kuhusu pepo na moto, malaika na mengi.

SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA

Soma hii aya kisha tafakari

(AL - BAQARA - 45)

Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kusali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu.

Msaada wowote kimaisha tumeambiwa kuupata ni kwa kusubiri na kusali(kuomba



Allah ALIYETAKASIKA) ila ni jambo gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu.

UBONGO wako unachochea uwezo wako kutoka ndani yako kwani uwezo na utashi wa utendaji(**will power**) inatokana na power ya UBONGO inayotokana na nafsi.

SAMAKI MMOJA AMERUKA KUFUATA CHAKULA, HUO NI MFANO WA WILL POWER

Unapoomba au kuswali kwa dhati basi uwezo wa kimaono(**vision power and psyche power**)unaongezeka.

Ukitamka jina la Allah lijulikanalo **Al jabbar** mara nyingi kila siku basi ubongo utakuwa na sifa ya kuhimili mambo na kufanya mtamkaji kwa dhati kuwa na sifa ya uhimili na kujiamini kwa uwezo wa Allah ulio na maana ya jina hilo la Al jabbar. Utakavyokuwa na yakini kuhusu uwezo wa Allah ALIYETAKASIKA ndivyo utakavyofaidika na nguvu ya maombi mahsusi (specific prayer) Kujua dua si hoja, bali muhimu zaidi ni namna ya kuzitumia na umakini utakaotumia katika kuomba.

Kuna watu wana silaha ila akitokea adui wanashindwa kutumia silaha hizo! Kuna watu wanajua mengi ila kuyafanyia kazi ni ngumu kwao. Hiyo ni power ya shetani na kundi lake kwa kichwa kilichokosa Dhikir, Kusoma QUR'AN, kukaa na udhu, kuleta ISTIGHFAAR na heri zingine za mutafuta radhi za Allah.

ALHAMDULILLAH ukiwa jitambua mapema na kutenda heri nyingi , kuna wengi wanaona bado maisha yapo ila wanashindwa kujua kuwa muda huu wa leo na sasa hivi ndio maisha yako! Kuna watu wanatoka nje kwenda kazini hata kabla ya kufika ofisini wanagongwa na gari wanakufa!



Kuna wengine usiku wamelala salama ila asubuhi ni MAREHEMU tayari! Kuna wengine wamelala wazima ila sasa hivi hawajitambui yaani stroke usingizini! Mengi yanayotunyemelea masaa 24 ila hatuyaoni na hatujui. Yote hayo usiyawaze zaidi bali wazia sasa hivi kufanya yafuatayo:

Kuleta ISTIGHFAAR mara nyingi, kutoa SADAKA kadiri UWEZAVYO, kutii amri za Allah, kumtaja, kumsifu na kumtukuza sana Allah na kusoma QUR'AN na kuifundisha pia. Heshimu maskini, jali yatima na wajane.

Kila juhudi yoyote katika heri Allah anaona, Mtume pia na waumini wanaona, kwa hiyo usijali wasemayo walimwengu.

Tutaendelea InshaaAllah na sehemu inayohusu Dua na nguvu yake ktk kutoa nguvu na mionzi mikali inayounguza yaani laser beam pia athari ya dua ndani ya ubongo, nafsi na mwili mzima

SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI

DUA YAANI MAOMBI YA DHATI KWA ALLAH YANAPROGRAM UBONGO NA KUBORESHA MAISHA YA MUOMBAJI

Soma QUR'AN

(AL - BAQARA - 186)

Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka.

Katika aya hiyo ,yeye wa pekee ARRAHMAN anasema yuko karibu kwa muombaji na ataitikia kila mja endapo atamtii yeye Allah wa pekee kwa kutenda mema na kuacha maovu.

ARRAHMAN hapa Duniani ugawa rehema kwa kila mtu kwa kipimo alichopanga yeye.

Hii ndiyo maana hata washirikina, makafiri na wengine wanapata riziki ikiwemo hewa ya oksijeni bure kama haki yao hapa duniani.

Mitume na manabii walitumwa kwa nyakati tofauti kufikisha ujumbe wa Muumba wa kila kitu na baadhi ya watu wakawatii na wengine wakakufuru, waliokufuru watapewa adhabu na ARRAHMAN mwingi wa Rehema baada ya kufishwa na wengine upewa hapa hapa duniani na kisha baada ya kufishwa.

DUA MAHSUSI YA DHATI

Dua ni ibada kwani Allah anasema kumuomba anapenda na kila siku ukimuomba yeye hata kuchoka kama sisi wanadamu tunavyochokana. Mzazi akipiga simu mara 2 anakuomba hela basi kila ukiona simu yake unahisi anataka hela na hupokei haraka wala kwa furaha, **kwa nini? Kama huna, unasema sina!**

ARRAHMAN hachoki kuombwa masaa 24. Dua mahsusi ni dua yenye malengo kwa muombaji.

Mfano : Maisha magumu

Dua mahsusi ni kuomba Allah akuwekee wepesi, mfano wa dua mahsusi ni dua kuhusu kuongezewa kipato na riziki upate ya kutosha.

Soma Suratil Waaqia'

Mtume alisema Suratil Waaqia' ikisomwa usiku baada ya Isha kwenye nyumba kila siku riziki itapatikana ya kutosha ili mradi juhudi ziendelee za kwaida na utendaji makini katika kutafuta riziki. Kumbuka pia ISTIGHFAAR inaongeza Rehema ya Allah na anatoa riziki kwa wahusika.

Astaghfirullah wa Atubu ilayh x 100 au zaidi ni maombi bora kwa Allah kuwa na huruma kwa muombaji.



Mfano mwingine ni Dua ya kujikinga na Shari mbali mbali wakiwemo wanadamu, majini na viumbe wengine.

Soma suratil Baqarah , Falaq, Nnasi , Ayatul QURUSIYYU kila siku asubuhi na jioni.

Ongezea dua hii pia

BISMILLAH ladhiy la yadhuru ma'a simi'i shaiun fil ardhwi wala fiy ssamaai wahuwa samiu' I aliim x 3

Ukidumu na udhu na ukatoa sadaka ukiweza hata kudogo kwa nia njema utakuwa na power ya kiroho hata ukiwa usingizini. Malaika wa ulinzi wa Allah watakuwa kazini na mionzi mikali ya kuunguza au kuharibu nguvu za shari yoyote

itakayokuwa inatokea endapo uadui wowote wa kijini na kibinadamu utafanyika .
Kumbuka usiwe muonevu wala mshirikina wala mzinifu wala mtenda maovu kila mara tena kwa makusudi.

Dua yoyote ukiomba kwa makini na kwa DHATI uleta athari kubwa kiasi cha muombaji alivyomtegemea Allah mmoja asiye na mshirika.

Ulishawahi kusoma Ayatul Qurusiya x 100? Au zaidi?

Suratil Falaq x 300?

Suratil Nnasi x 300?

Kumswalia Mtume x 1,000

Yaani

ALLAHUMMA swali ala Muhammad wa a'la alih Muhammad x 1000?

Ukipata nafasi jaribu. Utaona mengi na uwezo wa Allah utaonekana ukianza kuzisoma na kutaja kwa makini hata kabla hujasoma zaidi ya mara 200 utasikia mwili una nguvu mpya na uenda ukapata vitisho vya ajabu kabla hujamaliza kusoma sura hizo kufikia mara 300 . Usiache endelea mpaka mwisho ndipo utapata jibu halisi ya power ya dua mahsusi katika kuupa ubongo nguvu na nafsi ya mhusika.

Tutaendelea na Dua zaidi za kukupa nguvu kiubongo na kimaono ili utende kila jambo kwa kujiamini kwani kumtegemea Allah ni jambo kubwa.


SEHEMU YA ISHIRINI NA TATU

KUUPROGRAM UBONGO WAKO KWA DUA ILI UWE NA ULINZI WA ALLAH MASAA 24.

Soma Ayatul Qurusiya x 3 au zaidi kila baada swala na wakati wa kulala.

Matamshi

Bismillaahir Rahmaa-nir Raheem



Ayatul QURUSIYYU ina MANENO mazito ya Allah na ukiisoma kwa dhati mara kadhaa unatengeneza uwezo wa mionzi mikali ya laser yaani laser beam inayounguza nguvu zote zisizoonekana zilizo na uadui dhidi yako. Majini wa kushetani na binadamu wenye uadui wa kichawi na husuda mbaya dhidi ya kila anayesoma mara kwa mara QUR'AN, suratil Falaq, Ayatul QURUSIYYU ni hatari kwao ili mradi usimshirikishe Allah, usizini na jizuie na madhambi makubwa. ISTIGHFAAR kila siku mara nyingi na kabla ya kulala samehe kila mtu. Usiache kutoa sadaka hata tende au kipande cha mkate, usimkaripie au kumjibu vibaya anayeomba . Ukiwa huna cha kumpa basi ongea naye VIZURI .

Dua ni silaha ya Muumuni

Unaposoma dua na kuirudia mara kwa mara unaongeza uwezo wa UBONGO kutoa mionzi mikali hata ukiwa usingizini. Yaani hii inaitwa psyche power

Psyche power uwezo wa kuota na ukakumbuka ndoto, kuota nyoka unawapiga au kuwakwepa kukuuma au kuota unapigana na watu umelala, kuota unakimbizwa ila haukamatwi na adui au mnyama anayekukimbiza.

UBONGO ni hazina na ukiuprogram kwa dua , dhikir na kanuni nilizotaja kuanzia sehemu ya kwanza hadi sehemu ya 22 utashangaa mambo mengi uliyokuwa hujawahi kuona au kusikia.

BISMILLAH RAHMAN RAHIIM ni aya yenye maana kubwa.

Maana ya BISMILLAH ni Kwa jina la Allah, RAHMAN RAHIIM mwingi wa Rehema mwenye kurehemu.

Tafsiri yake hiyo imesheheni uwezo mkubwa!

Ukitamka mara nyingi BISMILLAH RAHMAN RAHIIM kwa dhati na kuweka kichwani maana ya BISMILLAH RAHMAN RAHIIM utauprogram UBONGO wako kwa sifa ya maana ya matamshi ya BISMILLAH RAHMAN RAHIIM na hapo ndipo utazidisha power ya UBONGO wako, nafsi iliyotulia na mwili uliotengamaa.

Ujinga ni janga(Ignorance is tragedy) kwani ujinga hauondoki kwa mtu kwa kuwachukia wanaofundisha bali kwa kusoma na kupata maarifa.

Allah kataja ujinga mara kadhaa ndani ya QUR'AN, pia mtume kasisitiza kufuta ujinga kwa kupenda kujifunza.

Kila nchi duniani sasa hivi inapanga bajeti kubwa kuelimisha watu kuanzia watoto shule na wafanyakazi kwa kuwapa kozi fupi, semina , warsha na kuwaongezea ujuzi kwa gharama kubwa.

Yote hayo ni KUUPROGRAM KUUPROGRAM UBONGO uwe aseti zaidi kuliko kuwa LIABILITY.

Liability maana yake ni deni, ubongo deni ni UBONGO wa mjinga.

Dua au aya au jina lolote la Allah ukiwa na dhamira katika kuomba na kujua maana ya unachotamka ndivyo matokeo yanakuwa makubwa kiasi kwamba UBONGO unajiprogram kwa maana halisi ya unachotamka kwa dhati kutokea

moyoni. Allah ALIYETAKASIKA yuko karibu kuliko hata mshipa wa shingo. TUZIDISHE uwajibikaji na Kumuomba kila mara.

Tafakari maudhui ya tafsiri ya Ayatul QURUSIYYU:

(AL - BAQARA - 255)

Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo yote milele. Hashikwi na usingizi wala kulala. Ni vyake pekee vyote viliomo mbinguni na duniani. Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao; wala wao hawajui chochote katika vilio katika ujuzi wake, ila kwa atakalo mwenyewe. Enzi yake imetanda mbinguni na duniani; na wala haemewi na kuvilinda hivyo. Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye Mkuu.

SEHEMU YA ISHIRINI NA NNE

UBONGO uko ndani ya kichwa na ndio maana Boda Boda lazima awe na kofia mbili, moja yake na ya pili ya mteja atakaye mbeba. Ubongo muhimu sana, mtu asiuvuruge jamani²

QUR'AN ni neno la Allah aliyeumba kila kitu

Jeshi mojawapo la Allah kutokana na kumtegemea laweza kuwa hili hapa.

Malaika 5,000 si MCHEZO! SUBUHANNAH LLAH.

Soma kwa makini kisha TAFAKARI!

(AL I'MRAN - 125)

Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkamchamngu na hata maadui wakikutokeeni kwa ghafila, basi hapo Mola wenu Mlezi atakusaidieni kwa Malaika elfu tano wanao shambulia kwa nguvu.

Dua za dhati katika hali yoyote Upata nguvu kubwa kutoka kwa Allah. Hii inatokana INATOKANA UBONGO kuwa na nguvu kimaombi na kifikira wakati wa kuomba dua .

Ubongo unaccontrol mwili mzima wa mwanadamu.

Mishipa midogo ikiwemo nuerones na nerves ni kama waya za umeme zinazosafirisha mawasiliano mwili mzima.

UBONGO KUUPROGRAM zaidi ni faida ya kila mwanadamu kwa kila nyanja ya kimaisha.

Duniani ukifanikiwa ni vita, ukifeli ni furaha kwa baadhi ya waliokuzunguka!

Kwa nini Mtume Rehema na amani za Allah ziwe juu yake alikuwa akiomba dua kila mahala, kila kitendo. Mfano kutoka nje alikuwa akiomba, kula , kulala, kupanda kipando, kushuka, kuingia chooni, bafuni, kuvaa nguo, kuingia mji wowote, kupanda mwiniko, n.k. yaani Mtumie wa Allah alikuwa anaomba dua hivi!!

Je mimi na wewe si tunapashwa kuomba dua zaidi?

UBONGO wako, nafsi yako na moyo wako vyote vinashirikiana kuendesha mwili mzima ila dereva ni UBONGO ndo maana hata boda boda anaambiwa awe na helmet mbili za kulinda kichwa yaani ya kwake na abiria, asipokuwa nayo ni adhabu yaani kichwa kina ubongo mali muhimu. Kofia kuivaa ni suna katika uislamu kwani inafunika kitu kilichohifadhi UBONGO. Wanawake katika uislamu kuacha kichwa wazi ni kosa na hata manaswara unaona masisita na maaskofu, mapadri wanafunika vichwa . Hiyo ni kuonyesha umuhimu wa kichwa ambapo UBONGO umo.

Dua inauprogram ubongo kwa uwezo wa Allah na kuulinda usivurugwe na Ibilisi, majini na wachawi. Dunia ya sasa silaha yako kubwa ni dua, ucha Mungu na kuamrisha mema na kuzuia maovu

Anasema Allah ALIYETAKASIKA

(AL I'MRAN - 104)

Na uwe kutokana na nyinyi umma unao lingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio walio fanikiwa.

Hivi unafikiri mlinzi wa nyumba yako anaweza kumkamata ibilisi, jini au mchawi usiku?

Hapana , wala bunduki haiwezi mgundua mchawi au mnafikiri na kudhibiti madhara yake!

Allah ndiye anamjua kila adui wa mwanadamu haswa! Ukiwa KIONGOZI, au mfunyabiashara wa viwango au uliyefanikiwa zaidi basi tambua shari za husuda zipo. Hii ni QUR'AN imesema " Shari za mwenye husuda anapohusudu"

Shari hizo ni nyingi mno.

Ukitaka kuwa mdogo na usiwe na lolote la mfano duniani basi ogopa husuda! Lakini ukiwa na bidii zenye tija jiandae kwa husuda na USIOGOPE ila utawaenjoy ikiwa utamtegemea Allah. Utawaona wenye husuda kwa maneno na hata ukiwa umelala utawaota mara kwa mara wanakuhoji, wanalalamika, wanakuita na hata mnapigana.

Ukiuprogram UBONGO wako kwa heri, QUR'AN, dua, sadaka, ISTIGHFAAR, dhikr na kukaa na udhu muda mwingi wataipata fresh na kudhalilika live. Amini usiamini ukweli ndio huo.

SEHEMU YA ISHIRINI NA TANO

KUUPROGRAM UBONGO KWA KUTAMKA MAOMBI SAHIHI

Kurudia neno(repetition) mara kadhaa lenye maana fulani ufanya UBONGO wa anayetaja utengeneze tabia yenye maana ya neno hilo. Mfano

Ukitamka neno **FURAHA** mara nyingi utaondoa stress na mfazaiko kimaajabu

Ndio maana ukimtembelea mtu mwenye story za lawama na kukatisha tamaa utashangaa ukitoka kwake huna mood yaani uko dhaifu na utajihisi umechoka! Ni sababu ya maneno yake!

Ukiwa huna mood ukakutana na mtu mwenye stori za kukupa moyo, FURAHA na matumaini utashangaa unakuwa na nguvu na moyo wa matumaini na mood inapanda kiasi kwamba utadhani kakupa dawa.

Matamshi ya dhati yana nguvu sana isiyoelezeka , kuna msembo kuwa maneno yanatengeneza kitu.

Omba kwa Lugha unayoimudu vizuri kwani Mungu wa pekee anajua nia yako na kila lugha.

Mfano umetingwa na mitihani ya kimaisha!

Tamka kwa dhati mfano kwa kusoma kiarabu na tafsiri au tafsiri pekee kama hujui kusoma kiarabu.

BISMILLAH RAHMAN RAHIIM

*(ASH-SHARH' - 6)

Hakika pamoja na uzito upo wepesi.

Pia tamka maneno haya ukiwa katika hali ya sintofahamu kimaisha yaani hali yoyote ile . Tamka maneno hayo kwa dhati.

Ya Hayyu Ya Qayyum, Birahmatika Astagiithu, Faagithiniy

Hayo maneno ni kumuomba Allah muweza aliye hai kwa Rehema zake akuokoe kwenye sintofahamu yoyote.

Soma hayo maneno mara nyingi mpaka ujisikie vizuri na nafsi imetulia.

Ukiweza soma Sura nzima. Kama hujui kusoma kiarabu soma maana na kuyatia maanani kwa dhati ila tafuta muda ujifunze kiarabu ili uwe unasoma na kuelewa maana ili maana yatafsiriwe na UBONGO na ndipo itatokea una chodhamiria kwa ridhaa ya Allah ALIYETAKASIKA . AI AZIIZU AI HAKIIM ni muweza wa kila kitu MTEGEMEE.

Pointi kubwa hapa ni jinsi ya kuprogram UBONGO ili nafsi, moyo na mwili uwe na power zaidi

Kila unalotamka UBONGO unalifanyia kazi na kukopi tabia na nguvu husika kutokana na maana ya neno au maneno. Rudia sana maneno mazuri yenye kuchochea hali na matumaini utajisikia na hali mpya.

ALHAMDULILLAH

Kila siku soma aya hii mara nyingi asubuhi na jioni na mahala popote . Hakika hii aya ina maneno mazito na ilishuka kwa Mtume Muhammad Rehema na amani za Allah ziwe juu yake kumponya na kupambana na Shari zote, wachawi, wenye husuda na shari za usiku unapoingia .

Usiku una mengi na giza kweli linabeba. Anasema muandishi wa tamthilia Meeting in the dark yaani watu wanafanya mengi gizani.

Soma Sura hii kila siku angalau mara 3 asubuhi na jioni . Soma kwa makini na kuhakikisha maana yanaingia kwenye UBONGO na nafsi yako inahisi ukubwa wa Allah aliyeshusha QUR'AN tukufu.

BISMILLAH RAHMAN RAHIIM

(AL - FALAQ - 1)

Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa mapambazuko,

(AL - FALAQ - 2)

Na shari ya alivyo viumba,

(AL - FALAQ - 3)

Na shari ya giza la usiku liingiapo,

(AL - FALAQ - 4)

Na shari ya wanao pulizia mafundoni,

(AL - FALAQ - 5)

Na shari ya hasidi anapo husudu.

Kumbuka

Kila unapotamka neno lolote linacopy tabia ya maana ya neno hilo ndani ya UBONGO na kisha matokeo ndani ya maisha yako!
Sasa Tamka maneno mazuri na yenye maana nzuri kwa mustakabali wa maisha yako!

Usitamke MANENO kama

"Siwezi"

"Hali mbaya sana"

"Nipate wapi pesa ya kuhiji "

"Mimi siwezi nunua Nyumba"

" Mtoto wangu hawezi fanikiwa "

"Sitafanikiwa , nimezeeka"

Na mengi kama hayo ya kujimaliza kimaisha. Acha kabisa kutamka MANENO hasi.

Tamka kama haya

"Ninajitahidi KUKAMILISHA mradi mkubwa"

" Mungu namshukuru kunipa akili"

"Muda wowote nitafanikiwa kupata pesa ya kutosha"

"Watoto wangu wanajitahidi sana kusoma na watafanikiwa"

"Nimeumbwa kufanikiwa"

"Sitaacha kujaribu hadi nifanikiwe, InshaaAllah "

Hayo ni mfano tu. Kuna kauli nyingi chanya mnazijua na zitumie.

Fikiria, Panga na kisha ifanyie kazi mipango bila kuacha au kukata tamaa hata ikifeli , rudia tena na rekebisha mara na kisha ENDELEA .

Mradi bado tupo hai, tunaweza fanya mengi na makubwa. Wajibika na uliza, soma na angalia mbinu za waliofanikiwa na boresha UBONGO wako kwa kuomba sana , kumtaja Allah sana, kuamka mapema na kufanya kazi kwa JUHUDI na maarifa bila kupoteza muda katika KULALAMIKA na kuona kuwa umechelewa. Aliyechelewa ni yule aliye kaburini.

SEHEMU YA ISHIRINI NA SITA

Ukisikia kichaa, unaelewa haraka haraka kuwa kichwa ndio kimevurugika.

Kichwani kuna UBONGO na ndio maana Lazima tuvae Helmet tukiwa tumepanda piki piki na tukiwa kwenye kazi za ujenzi.

KUUPROGRAM UBONGO ili tuwe BORA zaidi ni sifa ya UBORA aliotaja Allah ALIYETAKASIKA. Kichwa kikiwa vizuri tutaweza kuamrisha mema ndani ya jamii na kukataza maovu.

Soma QUR'AN, aya hii

(AL I'MRAN - 110)

Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu.

.....

Waislam tutakuwa BORA zaidi kukipata maarifa ya dini na dunia kisha tukaelimisha heri na kuamrisha mema wenzetu na tukawakataza maovu kwa maneno na vitendo vyetu sisi wenyewe.

Kuswali ni heri, Kufunga ni heri, kutoa zaka ni heri, kuacha fitina ni heri, kutoa sadaka ni heri, kusoma QUR'AN na kuizingatia ni heri, kusaidia ndugu ni heri, kuwaheshimu watu na haki zao ni heri, kuwalisha masikini ni heri, kuwajali na kuwatunza mayatima ni heri, kumuheshimu masikini na yoyote ni heri, kuacha zinaa ni heri, kuacha riba ni heri, kuacha husuda mbaya ni heri, kuacha uchawi ni

heri,kuacha pombe ni heri, kuacha shirik zote ni heri, kufanya Dhikir asubuhi na jioni na muda wowote ni heri, kumswalia mtume ni heri, kuchinja kwa ajili ya Allah ni heri, kutokuwa na chuki na KINYONGO ni heri, kula wastani na kuzingatia afya yako ni heri, kuacha kusengenya ni heri, kuacha kiburi ni heri. Mengi ya heri tunayajua na tuwakumbhshe wengi na tutakuwa UMMAH bora.

Mfano wa kulinda kichwa (UBONGO) na tija yake!

Jamaa mmoja mwezi wa pili mwaka 2022 alipata ajali ya pikipiki na alikuwa amevaa Helmet na kuifunga vizuri.

Maajabu alianza kichwa chini na Helmet ilipasuka kuanzia mbele hadi nyuma na kichwa chake kilibaki salama na UBONGO wake!

SUBUHANNAH LLAH!

Sasa fikiria kama asingekuwa amevaa Helmet ingekuwa vipi hicho kichwa na UBONGO uliomo?

Je kama angekuwa amevaa ile ya kutegeshea tu kwa kuogopa faini ya trafiki bila kuifunga vizuri si ingekuwa kitu kingine? Huyu angepasuka kichwa na UBONGO ukamwagika!

Tuendeleo kuvaa Helmet na kuzifunga vizuri ili kulinda UBONGO wetu endapo tutapanda au kuendesha pikipiki.

Nini chanzo kikubwa cha kuwa kichaa? Au Kuvurugika ubongo?

Kichaa yoyote akipelekwa kwa daktari uhojiwa na akiongea maneno yasiyoeleweka, Jamaa zake wakio naye na wanaomjua historia yake ndipo uhojiwa kuhusu tatizo la kichwa cha jamaa yao!

Baada ya hapo, daktari atataka kujua tabia zake na kuuliza kama anapata usingizi?

Je usingizi analala masaa mangapi?

Kama hapati usingizi , Dakari anauliza ni siku ngapi tangia hapati usingizi?

Basi hatua za kwanza ni vipimo vya maradhi mbali mbali ikiwemo malaria , kwa sababu kuna ukichaa wa kusababishwa na malaria sugu ya kuingia kwenye ubongo na kuuvuruga!

Daktari umpa dawa za usingizi kwanza kama haupati ili alale na kutuliza UBONGO.

Nini chanzo cha UBONGO kuvurugika na kukosa uwezo kiutendaji?

Nini chanzo cha Ugonjwa wa kichaa?

Nini chanzo cha stroke?

Kuepuka ukichaa na stroke kwa kanuni za kisayansi ikiunganishwa na dua mahsusi(specific prayer).

Allah ALIYETAKASIKA amewafundisha wanadamu mengi waliokuwa hawayajui!

Yote hayo yataelezwa kwa undani Toleo la 27 na 28 kwa tafiti za kisayansi zilizopo.

(AN-NISAAI - 85)

Mwenye kusaidia msaada mwema ana fungu lake katika hayo, na mwenye kusaidia msaada mwovu naye ana sehemu yake katika hayo. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza na ujuzi juu ya kila kitu.

SEHEMU YA ISHIRINI NA SABA

UBONGO UKIVURUGIKA NI HATARI SANA.

ALLAH ATUEPUSHE NA HILO

USHUHUDA WA KISAYANSI WA KWELI WA MADHARA YA UBONGO ULIOVURUGWA NA MARADHI YA AJABU

Anasimulia aliyekumbana na tatizo la UBONGO kuvurugika akiwa anasoma PHD **CHUO KIKUU NA KUWA KAMA MWANAFUNZI WA CHEKECHEA KIAKILI NA KUONEKANA KAMA UBONGO WA MTU WA MIAKA 70 WAKATI UMRI WAKE NI MIAKA 30. MBAYA ZAIDI AKAWA KAMA ZEZETA**

Kinachotokea kwa ubongo wetu, kwa upande mwingine, pia uonekana wazi kwa dalili za tabia na mwili kwa ujumla

Lakini vipi ikiwa kinyume chake kitatokea?

USHUHUDA WA KWELI, USOME KWA MAKINI

Mwanahabari Carolina Roatta anakabiliwa na ugonjwa adimu ulioathiri ubongo wake hadi kufikia hatua ya kuzeeka maradufu, ingawa mwili wake ni mchanga.

BBC Mundo inasimulia hadithi yake.



Nilipofikisha umri wa miaka 32 nilijihisi kama malkia wa dunia.

Ilikuwa Novemba 2012. Nilikuwa nimemaliza tasnifu yangu.

Nilikuwa nikifundisha katika chuo kikuu na nilikuwa nimemaliza kazi yangu iliyokuwa ndoto yangu ya mwandishi wa habari.

Siku nilipoenda kusaini mkataba wa ajira, nilifika nikiwa na uhakika sana hivi kwamba nilifanikiwa kuudhibiti ule mtikisiko ambao nilikuwa nao kwa muda mrefu.

Sahihi hiyo ndiyo ilikuwa jambo la mwisho nililoweza kuandika.

Uchunguzi wa kimatibabu

Kwanza mikono yangu iliruka kama mbawa za kipepeo, kisha kichwa na miguu yangu ikafuata.

Nilichagua kurekebisha utaratibu wangu.

Niliacha kuvaa blauzi za kubana na viatu vya kufunga, nikawa napenda jeans nyembamba, na hata nikaajiri msaidizi wa kuniandikia.

Wakati fulani pia nilianzisha shajara ya sauti ili kurekodi kila kitu kilichonipata.

Nilipinga kadiri nilivyoweza, lakini baada ya miezi sita hali ikawa ngumu.

Nilipitia miadi kadhaa ya matibabu ambayo ilidumu dakika 15.

Katika mfumo wa afya wa Colombia, unapaswa kupitia kwa daktari mkuu ili aweze kuagiza vipimo au kupeleka mgonjwa kwa mtaalamu.

Katikati ya hayo nilionekana na daktari wa neva kwa mara ya kwanza ambaye alibaini kimakosa na kudai nina tatizo la kutetemeka na kuniweka katika matibabu.

Dawa hiyo ilinituliza, lakini haikuondoa tetemeka..

Cha kushangaza, baada ya kushauriana na madaktari, wanasaikolojia, madaktari wa neva, ni daktari wa anayechunguza nishati mwilini ambaye alifikiria kuniagiza kipimo ambacho kingeonyesha picha za ubongo wangu.

Baba na mama walinisindikiza kwenye vipimo vya EMR.

Siku iliyofuata, tukiwa tunasubiri matokeo, nilipigiwa simu na mhudumu akiuliza ikiwa ninashughulika na kemikali kwenye kazi yangu.

Picha hizo zilionyesha kwamba ubongo wangu ulikuwa umelewa.

Wengine wa familia yangu walianza kuwa na wasiwasi.

Walinisaidia kupata mashauri wa kibinafsi na daktari wa neva mashuhuri.

Haikuwa rahisi lakini kwa mara ya kwanza nilihisi kwamba kuna mtu anaelewa kinachoendelea.

Uteuzi huo ulichukua saa tatu, daktari alinifanyia kila aina ya vipimo: Nilipaswa kugusa ncha ya pua yangu na kidole changu cha shahada, kuchora mviringo, kutengeneza vikaraagosi kwa mikono yangu, kusimama kwa mguu mmoja.

Katika zote nilianza kujikuna kichwa na kuishia kutokwa na jasho kana kwamba nimekimbia mbio za marathon.

Ilikuwa ni kama kufeli mtihani wa kuingia katika shule ya chekechea, lakini ikawa uchunguzi wa matibabu wenye kufariji.

Asante kwa vipimo vingine maalum, daktari wa neva alithibitisha kuwa nina ugonjwa wa Wilson.

Ni ugonjwa usiyo wa kawaida wa jeni iliyopewa jina la daktari wa neva aliyeufanyia utafiti, Samuel Alexander Kinnear Wilson, na unazuia mwili wangu usiweze kuchakata au kuyeyusha shaba.

Shaba?

Inatokea kwamba shaba ni kipengele kinachotusaidia kuwa na mishipa na mifupa yenye afya, pia inachangia kolajini na melanini kwenye ngozi.

Mwili wa mwanadamu hauzalishi, lakini huipata kupitia vyakula aina mbalimbali.

Lenti, mlozi, chokoleti, parachichi, kamba ... Orodha inaendelea.

Mwili huvunja vyakula hivi, ini husindika shaba inayotumia na kuondoa ile isiyohitaji, kwa kawaida kupitia mkojo.

Shida ni kwamba sisi tunaougua ugonjwa wa Wilson, badala na mfumo wa kumeng'anya shaba, hujilimbikiza hadi mwili hauwezi tena kupinga na kuanguka.

Kwa kawaida, ini huathirika zaidi, ikifuatiwa na ubongo, macho, na figo.

Lakini kesi yangu ni ya kushangaza zaidi.

Licha ya miaka 32 ya kujikusanya kwa shaba, ini langu lilikuwa sawa kiafya.

Ubongo wangu, kwa upande mwingine, ulizeeka mara mbili zaidi ya umri wangu.

Daktari wa magonjwa ya mfumo wa neva alisema inaonekana kama wa mzee wa miaka 70.

Pia nilikuwa na pete ya shaba karibu na mboni za macho yangu, ishara nyingine ya kawaida ya ugonjwa huo.

[OBJ]

Ugonjwa wa maisha

Watu wengi hugunduliwa kati ya umri wa miaka 5 na 35, lakini inaweza kuathiri vijana na wazee pia.

Ugonjwa huu hutokea wakati wa kuzaliwa, lakini ishara na dalili hazionekani mpaka shaba ikusanyike katika ubongo, ini, au kiungo kingine

Dalili na ishara hutofautiana kulingana na sehemu za mwili zilizoathiriwa na ugonjwa huo.

Inajumuisha: Uchovu, hamu ya kula, au maumivu ya tumbo - Ngozi kuwa na rangi ya njano na weupe wa macho - Macho kubadilika rangi ya hudhurungi - Kuongezeka kwa maji kwenye miguu au tumbo - Matatizo wakati wa kutoa hotuba, kumeza au uratibu wa kimwili - Harakati zisizo na udhibiti au ugumu wa misuli.

Ili kupata ugonjwa huo, ni lazima uwe na jeni yenye kasoro iliyorithiwa kutoka kwa kila mzazi.

Iwapo jeni moja isiyo ya kawaida itapokelewa, ugonjwa huo hauathiriwi, ingawa mtu atachukuliwa kuwa mbebaji na inawezekana kwamba watoto wake hurithi jeni hizo.

[OBJ]

CHANZO CHA PICHA,CRMR WILSON PARIS

Maelezo ya picha,
Pete ya shaba machoni ni moja ya dalili za Wilson

[OBJ]

Tiba

Matibabu ni pamoja na kunywa katika maisha yote utakayoishi duniani ambayo kwa kweli "huondoa" shaba ambayo hujilimbikiza kwenye viungo na kuiondoa kupitia damu na mkojo.

Daktari alinieleza kwamba itachukua muda kabla ya kupata nafuu, bila kutaja kama ingekuwa miezi au miaka.

Alinishauri nisiangalie mtandao ili asiniogopeshe na akabainisha kuwa dalili zingeongezeka ghafla wakati wa mwanzo wa matibabu.

Nilikuja kuamini kuwa itakuwa ya muda mfupi na kwamba baada ya muda mfupi ningeendelea na shughuli zangu.

Ukweli ni kwamba katika maisha yangu ya kila siku nilionekana kama "mtu mkubwa".

Nilitoka kuwa mwanamke mwenye uhuru mkubwa hadi kutegemea wengine katika kila nyanja ya maisha yangu.

Nilielewa muda mfupi baada ya utambuzi, wakati mama yangu alilazimika kunisaidia kupiga mswaki kwa sababu sikuweza tena.

Nakumbuka kabisa kwamba macho yangu yalijawa na machozi nilipofungua kinywa changu na akaanza kusafisha kinywa change kwa uangalifu kwa brashi.

Nililia kwa sababu nilihisi kwamba sikuwa na heshima tena.

Hangeweza kuwa mtu mzima, mtu binafsi.

Ndivyo nilivyohisi kila nilipohitaji msaada wake: alinisafisha nilipokojoa, nilioga, akanisaidia kubadilisha pedi nilipokuwa na hedhi, akanivalisha.

Baada ya karibu mwaka mmoja, alikuwa amefikia kikomo cha ulemavu unaoruhusiwa wa matibabu.

Hakuonyesha maendeleo yoyote ya kupata nafuu.

Hatua iliyofuata ilikuwa wao kunipa pensheni ya ulemavu.

Mwanzoni ilionekana kuvutia kwangu: kuwa na umri wa miaka 32, mshahara wa maisha, na kuweza kujitolea wakati kwa vitu vyangu vya kupendeza.

Lakini masaibu yalikuwa na upande mwingine: kuwa kijana na kujiona hana maana, kutupwa kwa ajili ya ulimwengu wa kazi, kupunguzwa na kuhukumiwa kupata mshahara wa chini nchini Colombia, ambayo wakati huo ilikuwa karibu dola 150 za Marekani.

Takwimu ambayo, sawa tu, ilinifanya kuwategemea wengine.

SEHEMU YA ISHIRINI NA NANE

UBONGO WAKO ULINDE USIVURUGIKE AU KUVURUGWA

Yanayovuruga Ubongo ni:

Kwanza soma aya hii

(AL - MAIDA - 90)

Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shet'ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa.

Pombe uvuruga ubongo.

Pombe ni mvuruga ubongo namba 1, ndiyo maana ALLAH kaizuia.

Mpaka mamlaka zote duniani zinazuia kuendesha gari au chombo chochote cha moto ukiwa umelewa.



Tunashuhudia mtu analewa anavua nguo kwenye watu bila aibu na mengi tunayaona ya kuhusu pombe na uvurugaji wa ubongo.

Bangi na madawa ya kulevya uvuruga ubongo

Bangi, Madawa ya aina zote ya kulevya pia uharibu moja kwa moja ubongo wa mwanadamu.

QUR'AN haijataja chakula cha kuvuta, imetaja kuleni kunyweni vilivyo bora na halali, sasa hii kuvuta bangi, sigara, n.k imetoka wapi?

Nyumba za vichaa wa bangi na madawa ya kulevya sasa ziko kila nchi!! Ubongo tayari umeishavurugika wanaprogramiwa upya wakiwa kambi kama watoto kwa gharama kubwa tena bila kuwa na wanalofanya.

Kupiga ramli

Hii ni kuvuruga ubongo kwa kuambiwa eti.mambo ya ghaibu na siri mbali mbali kuhusu maisha yako au ya watu au tatizo. Hii ni uongo mkubwa wa Shetani wa

kijini na wanadamu . MPIGA RAMLI, MTABIRI UWAGA HAWAJUI TAREHE YAO YA KUFA, ILA WANAJUA ETI SIRI!

Carin wakala wa shetani aliyewekwa kwa kila mtu na shetani tangia unapozaliwa umwambie shetani wa kijini baadhi ya sehemu ya maisha ya mpigiwa ramli na yeye umwambia mpiga ramli yaani mganga uambiwa na majini kutoka kwa jini mwenzao yaani carin unayekuwa naye maisha yote anaona baadhi ya mambo yako popote mko pamoja, mengine uongeza ya uongo na ndipo kichwa cha muhuisika uvurugika na kuwa mwoga kisha upewa masharti na gharama juu yake.

Wapiga ramli wanachonganisha jamii na kuvuruga bongo za watu wengi. Acha kuwasikiliza ila Omba ALLAH ALIYETAKASIKA sana na kila mara kwenye shida na raha atakupa majibu sahihi kupitia watu wema au ndotoni na utatuliza ubongo wako.

Kamari uvuruga ubongo kwa kufilisi watu na kuwafanya wawe masikini ghafla.

Kamari ni wizi na dhuluma kiasi kwamba wengine hawafanyi kazi za kuzalisha mali bali ushinda kwenye kamari na kubeti pia ni kamari.

Fuatilia anayebeti umsikilize maongezi yake utagundua kesho vurugika ubongo.

Acha kamari na kubeti utakuwa na ubongo salama.

Kuabudu majini, mizimu, masanamu yote ni kuwa mtumwa wa shetani , hii uvuruga ubongo kwani ukuondolea ulinzi wa ALLAH muweza wa kila kitu na kukutumikisha kwa masharti na hii uharibu ubongo kwani ukishaabudu mashetani na mizimu utaanza kuwa tofauti na wengine uanza kuwa wahu na kufanya maajabu na unyama. Mfano utamsikia mtu amebaka mama yake, mtoto wake, mbuzi, n.k eti anatafuta utajiri au cheo.

Mwingine anatoa kafara kwa mashetani watoto wake au mke wake au mume wake. Hii ni uharibifu wa ubongo wa hali ya juu. Jizui na tubu kama unafanya ili uwe na mwisho mwema.

Laana ya ALLAH kwa maovu na ukaidi uvuruga ubongo pia

Soma aya hii

(AL - MAIDA - 60)

Sema: Je! Nikwambieni yule ambaye ni mwenye malipo mabaya zaidi kuliko hayo mbele ya Mwenyezi Mungu? Ni yule ambaye Mwenyezi Mungu amemlaani na amemkasirikia, na amewafanya miongoni mwao manyani na nguruwe, na wakamuabudu Shet'ani. Hao ndio wenye mahali pabaya na wamepotea zaidi njia iliyo sawa.

Kuna waliogeuzwa moja kwa moja kutoka umbo la binadamu na kuwa nyani na nguruwe. SUBUHANNA LLAH, ALLAH tuhifadhi.

Kwa sasa kuna wanadamu wamevurugika ubongo na wana tabia zaidi ya nyani na nguruwe.

Allah atuhufadhi. Astaghfirullah

Wanafanya machafu bila aibu kuliko nguruwe, hii ina maana ALLAH analaani na kuwaacha wanakuwa kama nguruwe kitabia ila kiumbo ni binadamu.

Kwa hiyo ubongo unavurugwa pia na laana mbali mbali.

Tujikague na tuache maovu na uonevu kwa watu kisha tujirekebishe na tuombe msamaha kutoka kwa ALLAH yeye Al ghafaar , Attawabu, ARRAHMAN

ALLAH hana kinyongo anasamehe kila anayeirudi. Hii itatulinda ubongo wetu usivurugwe na laana za makosa yetu tunayojua na tusiyojua.

Wachawi na majini

Wanadamu wanavuruga ubongo wawenzao kwa maneno, uchawi, husuda, fitina.

Maneno mabaya uchochea fitina za aina zote. Kwa maana fitina za maneno na vitendo . Kuna fitina za vitendo.

Fitina ni mbaya kuliko kuuu mtu mmoja

Fitina inaweza kuuu wengi

Mbaya zaidi ni fitina kwani inaweza vuruga jamii kiasi kwamba watu wakauana mamilioni kwa mamilioni, mfano nchi za Marekani na Ulaya wanavyoingilia nchi zingine na kuhlalisha mapigano tena kwa fitina, kisha watoto, wazee na watu wengine wanauawa maelfu kwa muda mfupi, majengo yanabomolewa, miundo mbinu inaharibiwa na viwanda vinalipuliwa. Hii yote ni fitina imeanzia kwa mtu mmoja kisha wawili kisha kundi na baadaye maangamizi.

Sasa maajabu wanaoanzisha fitina wanakuwa mbali na uwanja wa mapambano wakichochea kwa mbali na wakijifanya wazuri wenye kujali watu na wenye huruma.

Fitina inavuruga bongo za watu kuanzia kwenye familia , taasisi, serikali na popote penye watu. Acha fitina utakuwa salama na jamii . Allah anasema fitina ni mbaya kuliko kua.

Uchawi na husuda vinavuruga ubongo

Uchawi umetajwa kwenye vitabu vyote vya dini kuanzia Taurati, Zaburi, Injili na QUR'AN

Chanzo cha uchawi ni husuda mbaya, ya kwa nini!? Ndio chanzo cha uchawi

Kila mchawi ana husuda na si kila mwenye husuda ni mchawi. HAPANA.

KUNA HUSUDA NZURI YA KUTAKA UMUIGE FULANI UWE KAMA YEYE AU UWE RAFIKI YAKE .mfano,

Mtu akiwa mcha Mungu na anaheshimu wajibu wa kila mtu, anachapa kazi na hana mzaha, basi ukipata husuda ya kuwa kama yeye bila kumdhuru hii ilo saaa. Sasa wengine wanamhusudu mpaka wanatamani neema imtoke, wanafikia kumloga pia. Allah ni mlinzi wako mtegemee bila wasi wasi kwa asilimia zote !



Dunia ya sasa uchawi ni kama malaria au zaidi ya malaria.

Kwa nini?: MAENDELEO ya sayansi na TEKNOLOJIA yanaongezeka sambamba na uchawi

Uchawi sasa unafundishwa vyuo vikuu vya ulaya, Amerika, Uk, Canada, South Afrika, n.k. kuanzia cheti, diploma, BACHELOR, masters , Phd.inafundishwa vyuo mbali mbali duniani.

Mpaka sasa mtandaoni unasoma uchawi kwa malipo au bure kwa kutumia mtandao wa internet. Allah atuhifadhi. SUBUHANNA LLAH.

Uchawi na wachawi wanajisifia kwenye mitandao KUANZIA Afrika, Asia, Ulaya bila aibu na wanatangaza wanavyoroga na kuvuruga vichwa vya watu kama ukitaka kulipiza kisasi au kukomoa jamaa au adui yako.

LINDA KICHWA YAKO ISIVURUGWE NA WACHAWI, Fanya haya

Soma QUR'AN kila siku

Juzuie na makundi ya ushabiki usio na tija

Funga saumu jumatatu na Alhamisi au zaidi

Fanya Dhikir kila mara

Kaa na Udhu

Toa sadaka

Simamisha swala na Sunna zaidi na za Usiku

Tamka ISTIGHFAAR nyingi

Mswalie Mtume mara nyingi

Wajali masikini, mayatima na wajane hata kwa kuongea nao na kuwapa matumaini pindi wakiwa na tatizo

Hakikisha kila jambo unaanza na BISMILLAH RAHMAN RAHIIM

Soma suratil Alhamdu(Fatiha yote kila asubuhi na jioni zaidi ya mara 4)

Allahumma SWALI ALA Muhammad x 11 au zaidi

Hasbunna LLAH WANIIMA li wakiyl x 7 au zaidi

Waombee wazazi wako

Rabbi ghafirily wali waalidayya Rabbi rahmuhumaa kama rabayan swagiirah x 3

KIsha jizuie na haya

Zinaa

Uchawi

Husuda

Uzembe

Pombe

Riba

Wizi

Kamari

Kusengenyua

Usiue

Ubakhiri

Ubinafsi

Kila siku leta ISTIGHFAAR nyingi kabla ya kulala hata kama huna kosa.

Mtume REHEMA na Amani za ALLAH ziwe juu yake alikuwa analeta Istighfaar mara 100 au 70 kila baada ya kusali. Yeye alikuwa ni Mtume, Je sisi? Sisi tulete nyingi sana.

Kama hujui kusoma kiarabu, jifunze dua na maana kwani UISLAM unaagiza kujifunza. Ukiwa unajufunza omba hata dua kwa kuswahili ili mradi imani na yakini ALLAH atajibu na utalindwa na madhara yote yasivuruge ubongo wako makusudi na hata wakijaribu utagundua haraka na kushugikia kwa njia sahihi.

SEHEMU YA ISHIRINI NA TISA

UBONGO UKIVURUGWA NA MARADHI, MAWAZO YASIYO NA MAJIBU(STRESS) NA MFAZAIKO(DEPRESSION) USABABISHA MWILI MZIMA KUATHIRIKA.



Huwezi kuondoa mawazo yasiyo na majibu kwa asilimia 100 bali unapunguza kwa kukabili na kushughulikia chanzo cha mawazo Hayo. Hakuna kitu chochote cha kudumu bali ni muda tu!

Subira imesitizwa ndani ya MAFUNZO ya uislam, ALLAH ALIYETAKASIKA anasema yuko na wenye kusubiri.

"Inna LLAH MA A' SWABIRIINA"

Subira yenye mpango maalum unaofanyiwa kazi hatua kwa hatua ndiyo inayosisitizwa hapa.

Isiwe subira ya kukaa tu na kusema sina la ziada na kusubiri uishilie. Nusura ya ALLAH ALIYETAKASIKA yuko karibu kwa yule anayeangaika kwa kusubiri na kusali. Dont settle!

Usione basi ndo mwisho wa kila na kulala, kisha unasema INNA LLAH MAA'SWABIRIINA.

Sasa Stress ikikosa mpango inamsababishia mhusika madhara makubwa ikiwemo

1. Kukosa usingizi au kusinzia kila mara hata kazini
2. Kupoteza kumbu kumbu haraka yaani kusahau kusiko kawaida
3. Kuishiwa ngubu mwilini.
4. Kutengeneza msongo wa mawazo na kuumwa kichwa

5. Kusababisha neva za ubongo kuzidiwa na kusababisha stroke ya ubongo(Brain stroke?)
6. Kugombana na kila mtu anaye mshauri au kumkosoa.
7. kutoshuriwa na kuwa mpweke
8. Kukosa uso wa bashasha na kuonekana uso umekasirika
9. Ikizidi na akakosa mazingira rafiki anajiua mhusika
10. Presha na stroke ya mwili utokea
11. Kuwa mlevi wa aina tofauti kupindukia kama pombe, bangi, madawa ya kulevya, sigara muda wote
12. Kusikiliza mziki , nyimbo muda wote.

Sahihi ni : SIKILIZA QUR'AN UTABORESHA UBONGO NA STRESS KUTOWEKA.

Kwa ujumla hizo dalili zinavuruga UBONGO badala ya KUUPROGRAM.

Mfazaiko ni chanzo pia cha mabadiliko ya mategemeo kimaisha kwani stress uzaliwa na mfazaiko wa muda mrefu na usio na majibu.

Tiba ya stress iliyo sahihi

1. Kabili chanzo cha stress

Mfano: ikiwa ni familia inasababisha kwa kukuudhi kila mara, waite uwambie madhara ya tabia yao kwako na uwashirikishe na ndugu wenye hekima wanaokupenda na kukuthamini

Kama ni madeni wambie wanaokudai kuwa huna pesa wakusamehe kukudai kwa shinikizo ili utafute kiasi na ulipe kwa awamu na usiwe ma bali nao kila wakihitaji kukuona.

Kama ni boshi wako kazini anakuandama bila kosa , mwambie kuwa anakupa stress na kama wewe ni mzembe acha uzembe na timiza wajibu wako ili usiandamwe na boshi.

Kama ni maisha, tafuta majibu kwa kubuni huduma zaidi ili upate pesa za kukidhi majukumu, usilalamike tu, kulalamika kuna haribu milango ya fahamu ya kufikiri na kubuni.

2. Pumzika kwa kupata muda wa faragha.

Kwa siku angalau saa 1 ukiwa pekee yako kwenye beach au shambani au chini ya mti wa kijani na maua au sinzia bila kusumbuliwa mahala patuivu.

3. Kuwa mbali na unao waita marafiki ila wana mtazamo hasi wa kila jambo

Kuna watu muda wote hawaoni zuri lako au maisha kwao ni kuona mambo yasiyopendeza au yasiyowezekana!

Kila jambo wana sababu nyingi za kukupa kuwa halitafanikiwa ila hawana ushauri wa njia za kulifanikisha.

Hawa watu tunao na wengine ni ndugu zetu, wazazi wetu na sehemu ya jamii yetu.

Hawa watu wanaondoa nguvu ndani yetu na bidii ya mambo yetu ikiwa tutawasikiliza kwa kila ushauri wao. Tusiwakubalie na tujitahidi kutokaa nao sana kwenye maongezi au kuwambia mipango yetu muhimu kwani tutakwama na kupata stress kutokana na kauli zao zisizo na afya kifikira.

4. Fanya mazoezi kwa kutembea sehemu za wazi (open space) na zenye mvuto wa kimazingira

Kukimbia au kutembea nusu saa kwa wiki x 5 inaweza kukuondolea mambo mengi yasiyo faa ndani ya mwili wako na stress pia kichwani mwako.

Kutembea ufukoni mwa ziwa, au mto au bahari au bustani au sehemu yoyote isiyo na msongamano usaidia nguvu ya kufikiri na kupunguza stress.

5. Tembelea watu wenye maono unaowajua na kuwapenda.

Kaa nao hata kwa kuwapa lunch ili mzungumze ,waombe appointment utapata kitu cha kukuondolea stress, wambie changamoto watakushauri na Ushauri uchukue na kuufanyia kazi.

6. Kunywa maji yaliyowekwa ndimu kila asubuhi nusu lita na jioni nusu lita

Hii itasaidia kufanya damu iwe nyepesi na kusafiri kwa wepesi, mishipa itapata nguvu zaidi na ubongo utapokea damu yenye oxygen yakutosha na utafunguka kichwa zaidi

7. Soma QUR'AN kila siku muda wa asubuhi na kabla ya kulala.

Tamka jina la Allah kwa lengo la kuomba Amani

Soma dua hii

Allahumma anta Ssalaam, waminika ssalaam , Tabarakta yaa zal jalaal wal ikram

Kisha, jina la Allah hili

Assalaam x 1000 au zaidi.

Usijaribu kukata tamaa na rehema za ALLAH ALIYETAKASIKA . Uliumbwa na kuwa duniani bila kuomba wala kuchagua. Kwa hiyo unaloona haliwezekani ni jepesi kwa aliyekuumba kutokana na maji yasiyo na kitu kwa kuangalia.

Duniani kuna mambo yaliyo wajibu kutenda kwa kila mwanadamu mazuri ikiwemo kumuabudu Mwenyezi Mungu. Basi tujitahidi na muda wote tuwe na mawazo ya matumaini.

SEHEMU YA THELATHINI

Vyakula vinavyoongeza nguvu za ubongo na uwezo wa kukumbuka



Ubongo ni muhimu sana kwa mwili na maisha ya binadamu. Ubongo ndio unahakikisha viungo muhimu vya mwili kama vile moyo na mapafu vinafanya kazi ipasavyo.

Ubongo ni muhimu sana kwa afya ya mwanadamu na hivyo ni muhimu kuhakikisha kiungo hicho cha mwili kinapata virutubisho vifaavyo.

Wengi wanahusisha ubongo na werevu wa mtu, lakini ubongo unafanya kazi kuhakikisha kuwa mwili wa mtu unaendesha shughuli zake ipasavyo. Kufikiri na kutafakari unahusiana na ubongo pia.

1. Samaki



Samaki wana virubisho vya asili kam omega-3.

Karibu 60% ya ubongo wa binadamu ni mafuta; na nusu ya mafuta hayo ni aina ya omega-3.

Ubongo wa binadamu hutumia omega-3 kutengeneza seli mpya za neva. Mafuta hayo ni muhimu kwa kumwezesha mtu kujifunza kitu na kukumbuka.

Kula samaki hata kwa wiki mara tatu utaona mabadiliko makubwa. Watu walioko karibu , mito na bahari ambapo samaki wanapatikana wakihitaji kusoma wanaelewa haraka na kuendelea mbele kielimu kwani ubongo una nguvu na kumbu kumbu ziko zaidi kwao.

2. Bizari manjano (Turmeric)



Kiungo cha curcumin kinachopatikana kwa bizari manjano kimethibitishwa kufaidi seli za ubongo, kupunguza msongo wa mawazo na kuboresha uwezo wa kukumbuka.

3. Broccoli



Broccoli ina viungo muhimu ikiwemo vinavyosaidia mwili kutoa sumu. Aidha, mboga hii imesheheni vitamini K ambayo utafiti umeonyesha huchangia kuboresha uwezo wa kukumbuka

4. Chai ya kijani kibichi (Green Tea)



Viungo vya caffeine vya L-Theanine vinavyopatikana katika chai hii vinamsaidia mtu kujihisi akiwa mtulivu

5. Njugu



Aina za njugu kama vile jozi, hazeli na lozi zimesheheni vitamini E na vitamini za kundi la B ambazo ni muhimu kwa kuboresha afya ya ubongo

5. Machungwa



Machungwa yana vitamini C ambayo ni vitamini muhimu katika kuzuia kudumaa kwa ubongo na kukua kwa seli zake. Machungwa yana kemikali ya flavanones ambayo husaidia kuimarisha ubongo wa mtu kukumbuka mambo upesi

6. Mayai



Mayai yana virutubisho muhimu vya ubongo ikiwemo vitamini B6 na B 12, folate na choline. Mayai yana vitamini D ambayo ni muhimu kwa afya ya ubongo.

7. MAPARACHICHI NA MATANGO



Watu wengi tunapenda matunda Fulani kwa ladha yake tuu bila kutaka kupata faida, Katika mwili ikiwa faida ya baadhi ya matunda ni pamoja na ladha yamatunda mabalimbali.

1. Tango ni chanzo kizuri cha vitamin B.
2. Tango huupa mwili na vitamin.

Asilimia 95 ya tango ni maji hivyo huupa mwili maji na kuusaidia kuondoa sumu mwilini kwani pia lina vitamin karibu zote ambazo mwili huhitaji kila siku.



Maparachichi ni muhimu kwani yana virutubisho vingi vya kujenga mwili ukiwemo ubongo. Usikose matango na maparachichi kwa wiki hata mara 3 kiasi cha tunda moja moja.



8. Ndizi mbivu na Tiki maji

Ndizi mbivu ni muhimu sana katika kuupa ubongo na tikiti maji, ila si

ruhusa kwa wenye kisukari ya kupanda kwani yana Glycemic Index kubwa sukari itapanda kwa kasi ukila nyingi.

9. Mboga za majani



Kabeji, karoti na mboga zingine za kijani zinasaidia kuupa ubongo power kubwa, usizikose

11. Karanga, korosho, Njugu mawe na mbegu za jamii ya kunde



Kuna protein ya kutosha kuupa mwili na ubongo nguvu na uwezo wa kufanya kazi, kuna virutubisho na mafuta asilia ndani ya karanga na korosho vya kuupa mwili nguvu ukiwemo ubongo.

Kumbuka Chakula ni muhimu katika afya yako kwa ujumla

Kula Dona, Mihogo, Viazi vitamu, Wali kiasi, Maziwa, Nyama kiasi, Nyama ya kuku, Samaki, Mboga za majani, kunywa maji safi na salama

Achana na kemikali ikiwemo vyinywaji kama pombe, soda, juice za bandia.



Jiulize kwa nini Hospitali zinaongezeka na pharmacy kila kukicha? Tena kwa wingi ni mijini . Wazee wa miaka 80 vijijini wako salama bila kisukari, presha, macho na wanatembea lakini mjini wengi wa

umri wa miaka 45 hoi na magonjwa kibao pamoja na kulala sehemu nzuri na kuishi maisha mazuri.

Sababau kubwa ni mfumo wa maisha na chakula wanacho kula kila mara. Wasomi wengi siku hizi wanapata maksi kubwa ila akili za ubunifu ziko chini, sababu kubwa ni aina ya vyakula . Ukila chips kuku wa kisasa aliyepewa madawa ya kumkuza kwa muda mfupi na wewe ukimla viini vya dawa vinakukuza haraka mwili na ubongo na unazeeka mwili na ubongo haraka kama kuku uliyemla kwa chips. Fuatilia ninayoandika hapa utapata ukweli.

Kemikali za kwenye kuku, nyama, juice na vitu vyote vya kuweka kemikali haziwezi kuacha watu salama kuanzia kiakili na kimwili. Nenda mhimbili au Hospitali kubwa utakuta clinic za aina tofauti za kisukari, presha, utumbo, moyo n,k, Zamani tulipokuwa tunasikia clinic tulikwa tunajua ni mama mwenye mimba au mwenye mtoto mchanga. Sasa ni tofauti wote ni clinic awe mama, awe baba. awe kijana. awe mzee.

Afya yako ndiyo mtaji wa kwanza, kuwa makini na acha kula kiholela mradi umevutiwa machoni kumbe ndani ya hicho chakula hakuna lishe.

Vyakula hivi si vizuri kiafya na ubongo wako utakuwa dhaifu ukizoea kuvila



